# NAFASI YA MWANAMKE: JINSI INAVYOTETEWA KATIKA NYIMBO ZA TAARAB ZA ZANZIBAR

**ELIZABETH KANGOGO YEGO**

**C50/68796/2011**

**IDARA YA ISIMU NA LUGHA**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**JUNI, 2013**

## IKIRARI

Tasnifu hii ni matokeo ya juhudi zangu za utafiti na si kazi ya mtu mwingine. Kazi hii haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu kingine.

MTAHINIWA

Sahihi ______________ Tarehe ________________________

Elizabeth K. Yego

Tasnifu hii imeandikwa na kutolewa ili kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

______________________ ___________________________

DKT. Omboga Zaja Tarehe

____________________ ____________________________

DKT.Rayya Timammy. Tarehe

## TABARUKU

Kazi hii ninamtabarukia marehemu mamangu  mpendwa Teresia Jepchumba, kwa juhudi zake za kunilea, kunielimisha, kunifunza haja ya uvumilivu maishani, kunishauri na kuniunga mkono kwa lolote nililoazimu kufanya.

iii

## SHUKRANI

Ninatoa shukrani zangu za pekee kwa Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na uwezo wa kukamilisha kazi hii.

Kisha, shukrani zangu zisizo na kifani zimwendee msimamizi wangu mahiri Dkt. Zaja kwa mawaidha na ushauri wake wa busara, mwongozo na masahihisho aliyonipa wakati nilipokuwa na vuguvugu la kutofahamu njia ambayo ningefuata katika bahari hii ya usomi na utafiti. Nampa hongera kwa namna alivyopitia sehemu mbalimbali za kazi yangu kwa makini na kuniwezesha kuukamilisha utafiti wangu kwa muda mfupi. Mawaidha yake mema yalinitia ari na mshawasha wa kuwaza, kutafakari zaidi na kuandika kazi hii. Ninamshukuru pia kwa kunipa maarifa kuhusu nyimbo za Taarab za Kiswahili na pia kanda mbalimbali za nyimbo hizi. Mola azidi kumpa hekima na neema zaidi.

Shukrani pia nazitoa kwa Dkt. Rayya ambaye hakuchoka kusoma kazi yangu mara kwa mara. Uhakiki wake pamoja na maoni yake ndiyo yaliyoupatia utafiti huu sura iliyo nayo. Kwa masahihisho na mawaidha yake namshukuru na kumwomba Mola azidi kumpa maarifa na neema.

Mbali na wasimamizi wangu, niliweza kupata ushauri wa kitaalamu na kiusomi kutoka kwa wahadhiri mbalimbali katika Idara ya Isimu na Lugha katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Nawapa shukrani kwa kazi bora ya mwongozo walionipa katika harakati yangu ya kusomea shahada ya uzamili. Miongoni mwao ni Prof. Habwe, Prof. Mberia, Prof. Wamitila, Prof. Abdulaziz, Dkt. Kineene wa Mutiso,Dkt.Mukhwana na Bw. Mung'ania. Ustadi na weledi wenu ndio unaonipa hamu ya kutaka kuendelea tena na tena.

Aidha, nawashukuru wenzangu ambao tulikuwa pamoja nao katika safari hii ya usomi ya shahada ya uzamili. Hawa ni Aziza, Alice, Jedida na Janepher. Mijadala kadha tulioshiriki na ushirikiano ulisaidia kurahisisha mambo yalipoonekana magumu.

Sitasahau marafiki zangu na dadangu Judith kwa kunipa usaidizi wa hali na mali wakati wa masomo yangu hasa katika kipindi kigumu cha utafiti. Wahisani hawa ni wengi lakini siwezi kuwataja wote ila nitamtaja aliyekuwa mwalimu mkuu wa shule ya upili ya Nakuru, marehemu Paul Kandagor aliyenipa motisha kwa miaka mingi ya kuendelea na masomo zaidi. Ninampa shukrani za dhati kutoka kwa moyo wangu. Heko na shukrani nawatunukia mume wangu, Ben Yego, watoto Ian, Byron na Maxwell kwa kuvumilia na hata kufadhili masomo yangu. Ningependa kumshukuru marehemu mama yangu Bi. Teresia kwa kuvumilia maisha magumu nilipokuwa nikiendelea na masomo yangu. Mungu amlaze pema peponi.

Pia, ninashukuru Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kuniamini na kunipa fursa ya kuendelea na masomo yangu ya shahada ya uzamili kikamilifu.

Mwisho, ninawatolea shukrani wale wote waliojitolea kupiga chapa tasnifu hii. Shukrani kwenu nyote ambao nimewataja na wale sijawataja, ninawatakia kila la heri maishani.

# MUHTASARI

Utafiti huu unahusu uchambuzi wa maudhui katika nyimbo za taarab za *Kibiriti Upele* na *Tupendane Wabaya Waulizane*.Nyimbo hizi ziliimbwa na Mwanaidi Shaaban na Mzee Yusuf.

Kazi hii imegawanywa katika sura sita.Katika sura ya kwanza tumeangazia maswala muhimu ya utafiti wetu.Tumeelezea swala la utafiti,madhumuni na nadharia tete zilizotuongoza.Aidha sababu za utafiti zimeelezwa pamoja na upeo na mipaka.Msingi wa nadharia wa utafiti umefafanuliwa na yaliyoandikwa kuhusu mada yalijadiliwa.Mwisho,mbinu za utafiti zimebainishwa na uchanganuzi wa data umefanywa.

Katika sura ya pili tulitanguliza kwa kueleza maana ya fani ya wimbo pamoja na kuzitolea maelezo ya aina mbalimbali za fani hii.Tumewarejelea wataalamu mbalimbali walioshughulikia fani hii.

Sura ya tatu na nne zimebainisha maudhui kwa kina katika nyimbo za *Kibiriti Upele* na *Tupendane Wabaya Waulizane* mtawalia.

Katika sura ya tano tumebainisha matumizi ya lugha katika kuwasilisha ujumbe wa waimbaji kwa hadhira.Sura ya sita ni hitimisho.Matokeo ya uchunguzi yalielezwa na mapendekezo ya uchunguzi zaidi yakatolewa.

## VIFUPISHO

**T.Y** **-** Tafsiri Yangu

**YALIYOMO**

IKIRARI ........ ii
TABARUKU ........ iii
SHUKRANI ........ iv
MUHTASARI ........ vi
VIFUPISHO ........ vii
YALIYOMO ........ viii
**SURA YA KWANZA:MAMBO YA KIMSINGI YA UTAFITI ........ 1**
1.0 Utangulizi ........ 1
1.1 Nyimbo za Taarab na Utungaji ........ 3
1.2 Tatizo la Utafiti ........ 5
1.3 Madhumuni ya Utafiti ........ 6
1.4 Nadharia Tete ........ 7
1.5 Sababu za Kuchagua Mada ........ 7
1.6 Upeo na Mipaka ........ 8
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ........ 8
1.8 Msingi wa Nadharia ........ 11
1.8.1 Utangulizi ........ 12
1.8.2 Nadharia ya Ufeministi ........ 12
1.8.3 Ufeministi wa Kiafrika ........ 15
1.8.4 Msingi wa Uhakiki wa Kimtindo ........ 18
1.9 Mbinu za Utafiti ........ 21
1.9.1 Ukusanyaji wa Data ........ 21
1.9.2 Uchanganuzi wa Data ........ 23
1.9.3 Umuhimu wa Utafiti ........ 23
1.10 Hitimisho ........ 23
SURA YA PILI: ........ 24
MAANA NA AINA ZA NYIMBO ........ 24
2.0 Utangulizi ........ 24
2.1 Fani ya Wimbo ........ 24
2.1.1 Umbo na Mtindo wa Nyimbo ........ 24

2.2 Maana ya Wimbo ........ 26
2.3 Aina na Dhima ya Nyimbo ........ 27
2.3.1 Nyimbo za Mapenzi ........ 29
2.3.2 Nyimbo za Harusi ........ 30
2.3.3 Nyimbo za Maadili ........ 30
2.3.4 Nyimbo za Sifo ........ 30
2.3.5 Nyimbo za Kusuta ........ 31
2.3.6 Nyimbo za Kizalendo/Kisiasa ........ 32
2.3.7 Nyimbo za Jando na Unyago ........ 32
2.3.8 Nyimbo za Dini ........ 33
2.4 Hitimisho ........ 34
**SURA YA TATU:MAUDHUI KATIKA KIBIRITI UPELE ........ 35**
3.0 Utangulizi ........ 35
3.1 Nafasi ya Mwanamke katika Ndoa ........ 36
3.2 Dhuluma za Mwanamke katika Ndoa ........ 37
3.2.1 Uasherati ........ 38
3.2.2 Usaliti ........ 39
3.3. Dhuluma za Kiuchumi ........ 39
3.4 Harakati za Kutetea Nafasi ya Mwanamke ........ 40
3.4.1 Talaka ........ 40
3.4.2 Uerevu na Umakinifu ........ 41
3.4.3 Uadilifu ........ 42
3.5 Nafasi ya Kiuchumi ........ 45
3.6 Hitimisho ........ 46
**SURA YA NNE:MAUDHUI KATIKA TUPENDANE WABAYA WAULIZANE ........ 47**
4.0 Utangulizi ........ 47
4.1 Mapenzi ........ 48
4.2 Majukumu ya Mwanamke ........ 49
4.2.1 Mapishi ........ 49
4.2.2 Maongezi ........ 49
4.2.3 Malezi ........ 49

4.3 Hitimisho........................................................................................................ 51
**SURA YA TANO:MATUMIZI YA LUGHA KATIKA KIBIRITI UPELE NA TUPENDANE WABAYA WAULIZANE ...................................................................... 52**
5.0 Utangulizi........................................................................................................ 52
5.1 Taarab ya Kisasa.............................................................................................. 52
5.2 Matumizi ya Lugha........................................................................................... 53
5.2.1 Lugha na Utamaduni...................................................................................... 55
5.3 Tamathali za Usemi katika Wimbo wa Kibiriti Upele........................................ 56
5.3.1 Tashbihi.......................................................................................................... 57
5.3.2 Kinaya/Kejeli.................................................................................................. 57
5.3.3 Misemo........................................................................................................... 58
5.3.4 Sitiari.............................................................................................................. 59
5.3.4.1 Bidhaa......................................................................................................... 60
5.3.4.2 Chakula....................................................................................................... 61
5.3.5 Takriri............................................................................................................. 61
5.3.6 Maswali ya Balagha........................................................................................ 62
5.4 Tamathali katika wimbo wa *Tupendane Wabaya Waulizane*............................ 63
5.4.1 Tashbihi.......................................................................................................... 63
5.4.2 Sitiari.............................................................................................................. 63
5.4.2.1 Cheo............................................................................................................ 64
5.4.2.2 Bidhaa......................................................................................................... 64
5.4.2.3 Chakula....................................................................................................... 65
5.4.2.4 Mimea......................................................................................................... 65
5.4.2.5 Ndege.......................................................................................................... 66
5.4.2.6 Michezo....................................................................................................... 66
5.4.3 Maswali ya Balagha........................................................................................ 66
5.4.4 Misemo........................................................................................................... 67
5.4.5 Takriri............................................................................................................. 68
5.5 Hitimisho........................................................................................................ 69
**SURA YA SITA:MUHTASARI WA MATOKEO ................................................... 70**
6.0 Utangulizi........................................................................................................ 70

6.1 Muhtasari wa Matokeo ........ 70
6.1.1 Upimaji wa Madhumuni ........ 71
6.2 Upimaji wa Nadharia Tete ........ 72
6.3 Changamoto za Utafiti ........ 74
6.4 Mapendekezo ........ 75
MAREJELEO ........ 76
KIAMBATISHO ........ 80
Wimbo 1. Kibiriti Upele – Mwanaidi Shaaban ........ 80
Wimbo 2. Tupendane Wabaya Waulizane – Mzee Yusuf ........ 82
Wimbo 3. Utalijua Jiji – Afua Suleiman ........ 85
Wimbo 4 Nyaubati – Rukia Juma ........ 88

## SURA YA KWANZA:

## MAMBO YA KIMSINGI YA UTAFITI

Kazi hii inaanza kwa kuangazia jinsi mwanamke alivyosawiriwa katika fasihi ya Kiafrika. Aidha mjadala kuhusu nafasi aliyotengewa mwanamke katika jamii inafanywa na kulinganishwa na ile inayobainika katika data zilizoteuliwa kwa lengo la kuonyesha jinsi nafasi ya mwanamke inavyotetewa katika fasihi simulizi ya jamii ya Waswahili. Pili, misimamo inayochukuliwa inatokana na mijadala na uthibitisho kutoka kwa mada. Mwisho mapendekezo mbalimbali yametolewa kutokana na matokeo ya uchunguzi ili tafiti zaidi zipate kufanywa kwa minajili ya kukuza fani ya nyimbo katika fasihi simulizi na kuziba mapengo yatakayobainika.

### 1.0 Utangulizi

Wasomi wa fasihi ya Kiafrika na anthropolojia kama vile Askew (2002) wanasema kwamba jamii ya Waswahili ilikuwa na mwingiliano wa muda mrefu na watu wa sehemu mbalimbali za ulimwengu hata kabla ya majilio ya Uislamu.Mwingiliano huu uliathiri utamaduni wa Waswahili kiasi cha kuifanya jamii kuiga na kuyafanya baadhi ya mambo kutoka kwa tamaduni zingine na kuzifanya kuwa sehemu ya utamaduni wao.

Mitagusano hii ya Waswahili na jamii zenye tamaduni mbalimbali iliwafanya Waswahili kuwa maarufu katika tamaduni zao. Athari za mitagusano hii zinabainika katika lugha yao mtindo wa mavazi na muhimu zaidi ni nyimbo zao. Mwingiliano huu umezungumziwa sana katika kazi ijulikanayo kama *Periplus of The Erythrean Sea*. Mtunzi wa kazi hii hajulikani lakini inasemekana kuwa ni mgiriki; anazungumza kuhusu kufanyika kwa biashara baina ya wenyeji wa pwani ya Afrika Mashariki na wachuuzi wa Kiarabu. Kazi hii ya Periplus, pia inaelezea

kuwepo kwa miji iliyostawi katika pwani na iliyofanya biashara na Wahindi, Waarabu na Wamisri. Athari za mwingiliano huu, zimefafanuliwa katika kazi hii.

Waswahili kama jamii zingine za Kiafrika walitumia nyimbo katika sherehe mbalimbali za jamii. Sherehe hizi ni za aina mbili. Aina ya kwanza ni za hatua mbalimbali anayopitia mwanajamii yeyote kama vile kuzaliwa na kupewa jina kwa mtoto, jando, harusi na kifo. Aina ya pili za sherehe zinahusu mambo ya kila siku kama vile kazi, mapumziko, michezo na mengine. Nyimbo katika jamii hii ni za aina mbalimbali muhimu ni zile za ngoma kama lelemama, chakacha, taarab na nyinginezo.

Wasomi wa fasihi na sayansi ya jamii kwa kipindi kirefu wamejadili maswala ya jinsia. Watunzi wa fasihi ya Kiswahili nao pia wameendeleleza mjadala huu katika kazi zingine za fasihi simulizi kama vile hadithi, misemo na nyimbo. Maswala yanayoangaziwa zaidi katika mjadala kama huu yanahusu ufeministi. Ingawa maswala ya ufeministi yanaendelea kubadilika kadri ya mpito wa wakati; maswala muhimu yangali yanathaminiwa. Na kwa kuwa wakati hudhibiti maswala yanayorejelewa utapata kuona kwamba yaliyoangaziwa katika miaka ya nyuma kama kwa mfano, kuchelewa kwa mwanamke kuolewa mapema lilikuwa ni jambo la aibu na lililowashughulisha wanajamii lakini hivi sasa swala hili halina umuhimu tena ila suala jipya kama la mwanamke kunyimwa haki ya elimu linashughulikiwa. Isitoshe, kuna maswala ambayo yanaendelea kudumu, hayo ni kama siasa, mafarakano yenye lengo la kupata madaraka, uhusiano wa kijinsia na tamaa ya umiliki wa rasilimali miongoni mwa maswala mengine. Maswala kama haya ndiyo yanaipa uhai kazi za fasihi.

Hakiki nyingi za kusisimua kuhusu taswira ya ufeministi, picha na maelezo ya kijinsia yamepata kushughulikiwa katika fasihi ya Kiswahili.Ijapokuwa ni hivyo, baadhi ya tafiti zilizofanywa kuhusu nyimbo za taarab na utendaji wake zinadhihirisha kwamba mazungumzo yote kuhusu taarab yanalenga pakubwa yanayowazingira wanawake.Jitihada za kujaribu kupigania sauti za wanawake kupitia katika nyimbo hizi zinabainika katika mawazo ya Fair (2001) , na Askew ( 2002).

**1.1 Nyimbo za Taarab na Utungaji**

Nyimbo za taarab zina historia ndefu. Historia hii ilianza katika miaka ya 1870 wakati utawala wa Sultan Seyyid Barghash kisiwani Zanzibar. Taarab, katika nyakati hizo inasemekana kuwa ziliingizwa nchini Zanzibar kama nyimbo za kumbi za watawala na ziliimbwa kwa lugha ya Kiarabu. Zilitumiwa kuwatumbuiza viongozi wenye asili ya Kiarabu, wafanyibiashara na mabepari. Waimbaji pamoja na ala za muziki ziliagizwa kutoka Misri na Uarabuni. Nyimbo hizi ziliendelea kutumia lugha ya Kiarabu hadi kufikia mwisho wa enzi za utawala wa Sultan Barghash ambapo lugha ya Kiswahili ilianza kutumika. Hadhi ya nyimbo hizi pia ilibadilika kutoka kwa wimbo wa walio na hadhi na wa tabaka la juu katika jamii na kuwa nyimbo za akina yakhe. Mabadiliko haya yanahusishwa na mwimbaji wa taarab aliyesifika sana Zanzibar na nchi za nje, Siti binti Saad, mwanamke wa asili ya Kitumwa (Fair ,2001 na Askew,2002).

Taarab ni mashairi simulizi ya Kiswahili yanayoimbwa. Neno taarab ni neno la Kiarabu lenye maana ya raha, starehe, furaha, burudani au kuingia ndani ya muziki Askew (2002:102-3). Kutokana na ufafanuzi wa Askew, tunaweza kusema kwamba taarab ni nyimbo za kuburudisha. Kulingana naye, waimbaji na watendaji wengi wa taarab ni wanawake na ni nadra sana kuwapata wanawake wakiwa watunzi ila utunzi hufanywa na wanaume.

Mjadala uliopata kufanywa kuhusu nyimbo hizi ni kwamba ufanisi katika utunzi una sifa moja muhimu na ya kipekee tofauti na aina nyingine za nyimbo. Sifa hii ni kuwa, watu mbalimbali wana majukumu tofauti tofauti. Mtu mmoja aweza kuwa mtunzi, mwingine wa kurekodi na wa tatu akawa mwimbaji. Kwa maoni yetu ushirikiano huu wa wanajamii katika utunzi na uwasilishaji wa taarab unaweza kutumiwa katika kutetea nafasi ya mwanamke katika jamii.

Fair (2001) na Askew (2002), wanakubali kwamba kimsingi nyimbo za taarab zilitungwa kuelezea maswala ya kijamii ambapo wanawake kama watunzi wanashiriki katika kubadilisha mikondo ya mijadala kuhusu ngazi za kijamii, jinsia na mahusiano ya kijamii kwa kuziweka katika vifungu vya nyimbo. Wanaendelea kusema kwamba mambo ya kibinafsi na ya umma hutungiwa nyimbo ambazo huimbwa kwa njia inayoonyesha kwamba maoni yanayotolewa yametoka kwa mwimbaji mwenyewe.

Matumizi ya tamathali nyingi ni sifa nyingine muhimu katika nyimbo hizi na hutumiwa kudhihaki tabia isiyokubalika na inayokiuka desturi za kijamii. Aidha nyimbo za taarab husifu, hukashifu, husuta na huonya dhidi ya wanaoonekana kuwa ni maadui wa mtu binafsi au jamii.
Jumbe katika nyimbo hizi zinatokana na uzoefu wa maisha, itikadi, mitagusano katika jamii na maisha yanayoenziwa. Isitoshe, jumbe huweza kuonyesha aina ya uhusiano uliopo kati ya jamii na asasi za kiutamaduni, mitindo ya mahusiano au matukio yanayofaa kukumbukwa.
Mwisho tabia za ulafi, uvivu, umbea, uvumi na matendo mabaya ya uasherati hushambuliwa katika nyimbo.

Kwa kuteua nyimbo mbili za waimbaji wa taarab, kazi hii imechunguza jinsi ambavyo nyimbo hizi zimetumiwa kutetea nafasi ya mwanamke. Uhakiki wa kina wa maneno katika nyimbo na utendaji wa taarab ya kisasa unaonyesha bayana kuwa kuna hisia ambazo zimekidhiwa au kuna zingine zimekosa kukidhiwa lakini hisia hizi hutajwa hadharani. Isitoshe nyimbo hizi zinaashiria hali mbalimbali za mitagusano na maongezi kuhusu maswala ya jinsia ya kike. Kimsingi, kazi hii inanuia kubainisha jinsi nyimbo za taarab zinavyotumika kutetea nafasi ya mwanamke katika jamii.

### 1.2 Tatizo la Utafiti

Maongezi kuhusu jinsia na yanayoizingira jinsia ya kike yamewavutia watunzi wengi wa fasihi. Wahakiki wengi wa fasihi waliozingatia maswala ya jinsia wamechunguza swala hili pasi na kushughulikia jinsia za kiume na kike kwa pamoja kwa minajili ya kupata kuzilinganisha. Lakini mara nyingi maswala yanayowazingira wanawake kama vile ukandamizaji wa mwanamke, sura ya mwanamke na nafasi ya mwanamke katika fasihi na jamii yameshughulikiwa. Katika hakiki hizi mwanamke amechorwa kama kiumbe duni katika mikabala mingi na kila wakati huwa chini ya mwanamume. Tumeweza kubaini kwamba mijadala mingi ya jinsia huangazia nafasi duni ya mwanamke na udhaifu wake na wala sio uwezo alionao. Kwa upande mwingine mwanamume amechorwa kuwa ndiye anayeendeleza dhuluma hizi za mwanamke.

Mabadiliko katika mahusiano ya kijinsia hayajafanyiwa uchunguzi ili kukidhi mahitaji ya mabadiliko ya nafasi za jinsia zote. Kwa maoni yetu nyimbo za taarab zinaangazia mitazamo mizuri kumhusu mwanamke kupitia kwa wanawake na wanaume. Mtazamo na uwezo wa mwanamke haujapata kufanyiwa marekebisho kuambatana na jinsi anavyochorwa katika kazi za watunzi wa hivi karibuni ndiposa kwa maoni yetu nyimbo za taarab ya sasa zinafaa ili

kubainisha nafasi mpya ya mwanamke kwa sababu kama tulivyotaja hapo juu, nyimbo hizi zimebadilika kutoka kwa taarab ya kale. Watunzi wa taarab ya sasa wamewasawiri wahusika wanawake wanaojiamini na wanaotetea haki zao, wamejinasua kutoka kwa minyororo ya utamaduni na kutoa mchango wao kuhusu maswala ya jamii zao sambamba na wanaume. Baadhi ya wanawake hao wamewapiku wanaume katika nyanja zinazohitaji nguvu za kimwili. Wahusika wa kike wenye uwezo mkubwa wanapatikana katika kazi za watunzi wa leo kama vile Lanina (Mazrui,1981) na Kazija (Mohamed,1980). Kwa upande mwingine kuna watunzi wa kazi za fasihi ambao wamewachora wahusika wa kiume wanaotetea nafasi ya mwanamke, hawa ni pamoja na Dewe (Mazrui,1981), Kabi (Mohamed,1980).

Kwa maoni yetu ni bora mabadiliko haya ya maisha yapate kujumuishwa katika uhakiki wa kazi za fasihi ili ufanisi upate kuonekana katika maswala yanayomhusu mwanamke na jamii kwa ujumla . Utafiti huu unanuia kupinga kasumba kwamba mwanamke ni mnyonge na ambaye lazima ajiegemeze kwa mwanamume ili apate kujikimu; mwanamke ana uwezo wa kupigania nafasi yake.

### 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu unadhamiria kuonyesha:

- Jinsi waimbaji wa nyimbo mbili teule za taarab wanavyotumia lugha ili kuendeleza maudhui ya uteteaji wa nafasi ya mwanamke katika jamii.
- Kwamba mwanamke amefaulu katika kutetea nafasi yake kupitia kwa nyimbo hizi.
- Kuwa jamii ikiwemo wanaume na wanawake imechukuwa jukumu katika kuitetea nafasi ya mwanamke.

- Ufaafu wa nadharia ya ufeministi wa kiafrika katika kuzichunguza nyimbo mbili teule za taarab.

**1.4 Nadharia Tete**

Utafiti umezingatia nadharia tete zifuatazo:

- Waimbaji hawa wamempa mwanamke mbinu mwafaka za kutetea nafasi katika jamii kupitia kwa maudhui na mtindo katika nyimbo zao.
- Mwanamke amefaulu katika kutetea nafasi yake katika jamii kupitia kwa nyimbo.
- Jamii bado imelegeza juhudi za kutetea nafasi ya mwanamke na ni lazima mwanamke mwenyewe ajizatiti ili aweze kutetea nafasi yake.
- Nadharia ya ufeministi wa kiafrika inafaa katika kuzihakiki nyimbo hizi za taarab.

**1.5 Sababu za Kuchagua Mada**

Wahakiki wa fasihi ya Kiafrika hasa fasihi andishi, wameonyesha jinsi mwanamke amekandamizwa katika jamii ya ubabedume na hata kumchora kama kiumbe dhaifu ambaye amekubali hali yake. Uhakiki wa aina hii japo umefanywa katika fani ya ushairi, nyimbo za taarab pia zinaweza kufanyiwa uhakiki wa aina hii.Ingawa uhakiki ambao tumetaja haujafanyiwa taarab,sisi tumechukuwa mkondo mwingine wa kuonyesha kwamba mwanamke amechorwa kama kiumbe mwenye nafasi yake na anaweza kutumia nafasi hii kujitetea katika jamii.Sababu nyingine ya uteuzi wa mada ni kuwa nyimbo za taarab huimbwa katika miktadha maalum kama vile sherehe za harusi na mambo ya utamaduni na wengi wa waimbaji wake ni wanawake.Hali hii ya kuihusisha taarab na wahusika wa kike ndilo lililotupa ari ya kuteua mada.

## 1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti huu umejikita katika maudhui ya nafasi ya mwanamke na jinsi inavyotetewa katika nyimbo za taarab za *Kibiriti upele* na *Tupendane Wabaya Waulizane* zinazoimbwa na waimbaji wawili, Mwanaidi Shaaban na MzeeYusuf.  Tumezipitia nyimbo hizi kwa lengo la kutambua na kueleza maudhui ya nafasi ya mwanamke. Azma yetu katika utafiti huu ni kutumia nadharia ya ufeministi wa Kiafrika kama nadharia ya kimsingi.Aidha tumechambua vipengele vya semantiki na sintaksia katika uhakiki wa kimtindo ili kuchunguza jinsi lugha ya nyimbo hizi inasaidia kuendeleza maudhui ya waimbaji. Tathmini ya mchango wa wataalam mbalimbali kuhusu nafasi imefanywa na pia mchango wetu umetolewa.

## 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Utafiti huu ni zao la kuzisoma tafiti mbalimbali zilizoshughulikia fasihi ya Kiafrika iliyoangazia maswala ya jinsia ya kike ili tupate msingi wa kuendeleza mjadala wetu. Udurusu wetu unadhamiria kuangazia fafanuzi mbalimbali za nyimbo kwa lengo la kuonyesha majukumu ya wahusika wa kike katika kubainisha malengo ya mtunzi. Matokeo ya udurusu huu yametusaidia baadaye kutathmini jinsi wahusika hawa  wanavyoweza kutumiwa kuangazia na kutetea nafasi za wanawake katika nyimbo za taarab. Pili, udurusu huu unanuia kumulika jinsi maswala ya nafasi ya mwanamke katika harakati za kijamii yalivyoshughulikiwa kupitia kwa lugha. Tatu, mawazo yanayotokana na udurusu wetu yametumiwa kueleza namna swala la ukandamizaji wa mwanamke lilivyopewa nafasi za pembeni na jinsi linavyoweza kupewa kipaumbele katika kuendeleza harakati za wanawake.

Wimbo katika msingi wamaelezo ya kamusi sanifu ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya muziki.Kwa kujikita katika uelewa huu, Beja (2001) anauona wimbo kama ni utungo wa fasihi simulizi unaowasilisha ujumbe kwa kutumia sauti na matendo ya waimbaji. Kwa kuzingatia sifa hizi, wimbo ni sanaa tendaji. Isitoshe, Beja anaona sifa nyingine ya wimbo ni kwamba huimbwa katika sherehe za aina mbili, rasmi na isiyokuwa rasmi na anaafiki maoni kwamba utendaji ni uti wa mgongo wa fasihi simulizi. Ufafanuzi wa Beja aidha unaafiki maelezo ya wimbo kuwa ni mashairi ambayo yanaimbwa kwa minajili ya kufanya kazi maalum. Uhusiano wa wimbo na mashairi unabainika wazi katika sifa zake zote isipokuwa kwamba njia ya kuwasilisha ni tofauti. Fauka ya hayo, anabainisha sifa bainifu ya wimbo kwamba unaimbwa na makundi ya watu ilhali ushairi unaweza kukaririwa au kughanwa na mtu mmoja.

Ufafanuzi huu wa Beja unaelekea kukaribiana na mawazo ya Timammy (2002) anayesema kwamba wimbo ni tamko lenye mahadhi na lililo na beti moja au zaidi zenye maana kikamilifu kimuktadha. Hii ina maana kwamba wimbo ni fani inayowasilishwa kwa mdomo na ina mpangilio maalum na ulio wa kipekee ikilinganishwa na fani zingine za fasihi kama riwaya na tamthilia. Nyimbo za taarab zina muundo wa beti na kila ubeti ukiwa unawakilisha ujumbe mbalimbali.

Miongoni mwa maswala yaliyopata kuzungumziwa kuhusu maudhui ya jinsia ya kike katika fasihi ya kiswahili ni pamoja na taswira, sura na picha. Taswira ya kwanza ya mwanamke ni kuwa kiumbe duni na mnyonge. Uhakiki kwa msingi huu unabainika katika Utendi la *Mwana Kupona* (1858), unamchora mwanamke kama kiumbe duni na anayejiegemeza kwa mwanamume. Utenzi huu unaendelea kudai kuwa ni wajibu wa mwanamke kumhudumia

mwanamume kwa unyenyekevu kwa kuwa mwanamume ndiye atatoa uamuzi kuhusu zawadi ya mke ahera. Taswira hii ilikuwa na nia ya kudumisha ukandamizaji wa mwanamke. Licha ya msimamo huu wa mtunzi hatuoni ushawishi wowote wa kinadharia kwa kuwa sababu za ukandamizi hazikutolewa.

Kazi nyingine iliyomchora mwanamke kama jasiri ni *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Mayasa amechorwa kama mwanamke jasiri katika vita. Kazi zingine ambazo zimemsawiri mwanamke kama kiumbe mwenye hadhi na anayefaa kuheshimiwa ni katika *Utendi wa Hati* na riwaya ya *Siti binti Saad*, zote za Shaaban Robert. Mtazamo huu unampa mwanamke msukumo na matumaini ya kutetea nafasi yake.

Mbali na ushairi na tendi, nyimbo za taarab zimepata kufanyiwa utafiti na baadhi ya wasomi na watafiti wa Kiafrika ambao wamebainisha kwamba nyimbo hizi zinazungumza kuhusu maswala mengi ya jamii kama vile ndoa, harusi na uchumi. Khatib (1992) katika uchunguzi wake wa historia ya taarab alidhihirisha kwamba nyimbo hizi zilikuwa zimebadilika kutoka kwa zilizokuwa zimeletwa na Barghash kuwa ni nyimbo za wenye uwezo na mali na baadaye zikawa za akina yakhe. Anaendelea kusema kwamba maudhui pia yalikuwa yamebadilika kutoka kwa yale ya kijamii na ya kutumbuiza na mengine yakaongezewa.

Uhakiki huu ni bora kwetu kwa kuwa unatupa fursa ya kujua historia ya nyimbo hizi. Kazi hii ni tofauti na kazi yetu kwa sababu yetu, inachunguza maudhui ya nafasi ya mwanamke na jinsi inavyotetewa.

Ufahamu wa Kingei (1993) wa nyimbo za taarab nchini Kenya ulionyesha utendakazi wa nyimbo za taarab kwa kuzingatia lugha, utamaduni, mawasiliano na maudhui. Uchunguzi wake wa maudhui katika taarab umetufaa katika utafiti kwa sababu utatupa msingi wa kuelezea jinsi nafasi ya mwanamke inavyotetewa pia taarab ni uwanja tulioushughulikia.Tofauti ya kazi ya Kingei na yetu ni kuwa,Kingei ameshughulikia maudhui kwa kina na nyimbo alizozishughulikia ni za Kenya ilhali sisi tumejikita katika maudhui ya nafasi ya mwanamke katika taarab ya Zanzibar.

Maswala mengine yaliyopata kushughulikiwa katika taarab ni pamoja na mitindo. Timammy (2002), katika kushughulikia nyimbo za harusi za Waswahili wa Mombasa kwa kutumia uhakiki wa kimtindo,amebainisha aina mbalimbali za nyimbo hizi.Kutokana na kazi ya Timammy,tulipata kuona kuwa kuna aina nyingi za nyimbo za Waswahili na taarab ni aina mojawapo. Ingawa uhakiki huu unahusu nyimbo za harusi za Waswahili wa Mombasa, ni tofauti na kazi yetu kwa kuwa sisi tunashughulikia maudhui ya nyimbo za taarab za Zanzibar.

Licha ya tofauti hizi, kazi hii imetufaa kutokana na hali kwamba imetuwezesha kujua aina zingine za nyimbo katika jamii ya Waswahili tofauti na taarab.

Utafiti huu unadhamiria kuonyesha kuwa mwanamke kupitia kwa nyimbo za taarab, amepata jukwaa muhimu ya kuwasilisha sauti yake.Mwanamke tayari ana uwezo na silaha za kujikomboa.

**1.8 Msingi wa Nadharia**

Nadharia ya ufeministi inashughulikiwa katika ngazi mbili. Kwanza, maelezo ya kijumla yatatolewa kuhusu ufeministi. Pili, ufeministi wa Kiafrika umejadiliwa kwa kuwa huu ndio

msingi wa utafiti wetu.Tatu,tumejumuisha uhakiki wa kimtindo.Vipengele vya kimtindo kama semantiki na sintaksia vitatumika hapa na pale katika kazi hii.

### 1.8.1 Utangulizi

Utafiti unajadili kuhusu nafasi ya mwanamke kama inavyobainika katika nyimbo za taarab. Kwa kuipa msingi maeneo ya kijiografia, utafiti umejikita katika ufeministi katika fasihi ya Kiafrika, eneo ambalo lilipuuzwa na waanzilishi wa nadharia hii. Maeneo ya Marekani, Uingereza na Ufaransa ndiyo yaliyoshughulikiwa tu, lakini eneo la Afrika lilizingatiwa na wanaharakati wa baadaye. Nadharia hii ya kifasihi ndiyo inafaa kutumika katika kuchanganua athari za utamaduni na mambo mengine ya kijamii yanayoathiri mahusiano ya kijinsia katika jamii za Kiafrika na watu weusi wenye asili ya Kiafrika lakini wanaopatikana sehemu mbalimbali nje ya bara la Afrika. Kazi pia imefanya uchunguzi wa kijumla kuhusu nadharia ya ufeministi wa fasihi na migawanyo yake huku kila sehemu ikipimwa kama inatosha kuzihakikia mambo ya kijinsia na mambo mengine yanayohusiana na nyimbo za taarab na ufasiri kwa kijumla.

### 1.8.2 Nadharia ya Ufeministi

Nadharia ya ufeministi inaaminika kwamba ilianza nchini Ufaransa katika karne ya kumi na tisa kama kikundi kilichokuwa kinapigania haki za kibinadamu za watu wachache katika jamii dhidi ya dhuluma kutoka kwa walio wengi.Katika msingi huo, wasomi waliojihusisha na Wollstonecraft (1792) walihusisha ufeministi na harakati za kupigania haki za kibinadamu za mwanamke. Harakati hizi zilianzishwa na wanawake wa rangi tofauti nchini Marekani katika karne ya kumi na nane. Kuanzia wakati huo, ufeministi umepitia mabadiliko mengi sana ya kiusomi.

Upiganiaji wa haki za mwanamke inasemekana ulitokana na azma ya wanawake wa rangi kutoka Marekani na ambao walipitia ukandamizaji mwingi chini ya tawala za ufalme za Waingereza. Utumwa na kutengwa kwa misingi ya rangi zilikuwa ni sababu maalum za kupigania ukombozi huu. Kutengwa kwa msingi wa rangi na kunyimwa haki za kibinadamu ndizo sababu za wanaharakati kufahamu kwamba njia ya kipekee ya kupata uhuru wa kijamii, kisiasa na kiuchumi ni kwa mwanamke kujisimamia kupitia kwa rasilimali.

Kipindi hiki ndicho kilikuwa ni wakati wanaharakati wa kijinsia walianza kusaili kuhusu miundo misingi ya kitamaduni yaliyoakisi haki za raia kulingana na rangi, mali na matabaka ya kijamii. Mawazo haya yalikuja kuwa msingi wa kampeni za kupigania usawa wa kijinsia katika sehemu mbalimbali za ulimwengu.

Maoni yametolewa kwamba kila binadamu anapozaliwa ana haki za kiasili za kuwa na uhuru na usawa ndiyo yayolichangia harakati za ukombozi.Mchango wa Magharibi katika ukuaji wa ufeministi ulitokana na waafrika walioishi Ulaya kujifunza kupiga vita udhalimu na ubaguzi wa rangi ulioendelezwa na wazungu dhidi yao. Maoni yanatolewa kwamba kuna tofauti kuu kati ya ufeministi wa Magharibi na wa Afrika. Ufeministi wa Magharibi, ulipigania haki za raia na ufeministi wa Afrika ulipigania haki za kibinadamu na kijinsia.

Mjadala unaoendelezwa na Wollstonecraft kuhusu ufeministi unatokana na mawazo yanayoendelezwa na wanaharakati wenye mawazo mapana na huru kwamba kila binadamu ana haki za uzawa ambazo ni uhuru na usawa. Anaendelea kusema kwamba jambo la busara ni kukubali kuwa mwanamke ana uwezo na akili sawa na mwanamume ikiwa walizaliwa wakiwa

na usawa. Tapo hili la ufeministi baadaye lilijulikana kama ufeministi huru. Aidha, inasemekana kuwa ni mzizi wa ufeministi unaopinga madai kwamba mwanamke anamtegemea mwanamume na kuendelea kusema kuwa mwanamke ana haki na nafasi duni. Mawazo haya yamekuja kutiwa nguvu na mawazo ya kisiasa yaliyoendelezwa na mabepari wa Marekani, Ufaransa na Uingereza.

Bressler (2003) anaeleza kwamba uhakiki wa ufeministi unaofaa katika fasihi ni ule unaojikita katika uhakiki wa usawiri wa mwili, lugha, akili na utamaduni. Baadhi ya vipengee hivi vimejadiliwa katika uhakiki wetu. Taswira ya mwili huwasilisha ujumbe hata ikiwa anayehusika amenyimwa haki ya kunena. Lugha ni njia muhimu sana inayotumiwa na binadamu katika kuwasilisha hisia na maoni. Akili hudhibiti matendo yote ya binadamu ikiwemo hali ya kiakili. Utamaduni umetumika sana katika utafiti huu kwa sababu utahakiki maswala ya kijinsia katika mtazamo wa utamaduni wa jamii za Kiafrika.

Lengo la kimsingi la utafiti ni kuelewa jinsi maswala ya utamaduni wa jamii yanavyoathiri uelewa wa wanawake na wanaume wa jamii wanamoishi na hata nafsi zao. Wafula na Njogu (2007), wanatoa maoni kwamba nadharia ya ufeministi hupigania kulinda haki za wanawake katika jamii ya ubabedume. Wanadai kwamba himili kuu la nadharia hii ni kubaguliwa kwa wanawake katika jamii kwa misingi ya jinsia yao ya kike. Hali hii inawaweka miongoni mwa wanyonge katika jamii.

Nadharia ya ufeministi inatiwa nguvu na hitaji la kubadilisha mtazamo huu wa utamaduni na kuimarishwa kwa nafasi ya mwanamke kama binadamu aliye na haki sawa na mwanamume. Ufeministi ni mkabala unaohoji itikadi za kiume ambazo zimekuwako ulimwenguni kwa kipindi

kirefu. Uchunguzi wa fasiri za kiume katika fasihi pia huchunguzwa kwa lengo la kupima fasiri hizi kama zinaendeleza itikadi za kiubabedume. Wahakiki wanaotumia nadharia hii wanahoji kuhusu sauti ambayo imetawala jamii kwa muda mrefu; sauti hiyo ni sauti ya mwanamume. Katika hali ya kutaka kuinua sauti ya kike, wanaharakati wengine waliojitokeza ni pamoja na Woolf, (1929), Wolltsonecraft (1792), Beauvoir (1949), Greer (1971), Eagletone (1991).

Beauvoir (1949) anashambulia asasi mbili za jamii zinazochangia ukandamizaji wa mwanamke Asasi hizi ni za ndoa na tamaduni. Anaendelea kusema kwamba dini inamfunza mwanamke kuwa mnyenyekevu; ndoa inampa mwanamume uwezo mkubwa akilinganishwa na mwanamke, nao utamaduni umemsawiri mwanamke katika njia iliyo hasi na duni. Anaendelea kusema kuwa kila jamii ulimwenguni ina nguvu fulani inayoiongoza na pia ina utamaduni wake. Tumefanya uchunguzi wetu kwa kutumia mawazo haya kama kigezo cha kupimia iwapo waimbaji waliotajwa hapo juu wamempa mwanamke nafasi anayostahili.

Utafiti huu pia umetumia dhana ya kuchunguza uandishi wa kike (*gynesis*) kama tapo la ufeministi. Mtazamo huu unashikilia kwamba watunzi wa kike wana lugha yao inayowawezesha kumchora mhusika wa kike kwa njia ya kumpa hadhi ya kutetea nafasi yake. Ukandamizaji wa mwanamke katika ndoa unabainika katika kazi ya Greer (1971) anapowashauri wanawake waisusie asasi hii kwa kukataa kuolewa. Anaamini kwamba mwanamke akikubali kuolewa anageuzwa kitu cha kumilikiwa na “kuwako” kwake hufutwa.

### 1.8.3 Ufeministi wa Kiafrika

Afrika ni eneo ambalo halikuangaziwa na wahakiki wa ufeministi wa Kimagharibi na ndio sababu Bressler (2003) amehusisha ufeministi na maeneo matatu ya kijiografia; Marekani, Ufaransa na Uingereza.

Ingawa ufeministi wa Kiafrika ulihusu maswala ya Kiafrika uliendelezwa na mataifa ya Kimagharibi kupitia kwa wanawake wa rangi nyeusi na wenye asili ya Kiafrika.Mwanamke katika jamii nyingi za Kiafrika amesawiriwa kama kiumbe duni na ametengewa nafasi inayoonekana kuwa ni ya chini lakini iliyo na majukumu mengi. Kwa msingi huu, utagundua kwamba mwanamke ambaye anathamini ndoa na watoto atakubali kudhulumiwa na mumewe kwa vyovyote vile ili kudumisha ndoa yake. Mawazo kama haya yanaendelezwa na Leslie Ogundipe katika Adeola (1990) kwamba,

> "Katika jamii ya ubabedume, mwanamke kwa kukusudiwa wanabebeshwa majukumu maradufu au zaidi ya yale ya wanaume" (T.Y).

Mwanamke anatukuzwa kwa kupewa majukumu mazito huku akiendelea kubaguliwa na kutengwa kwa maamuzi ya kijamii na hata kunyanyaswa.

Steady (1981), anasema kwamba ufeministi wa Kiafrika umejikita katika mwelekeo wa kuangalia majukumu tofauti ya kijinsia kama yanayoegemeana na kukamilishana. Anaendelea kusema kwamba majukumu haya yanaenda sambamba na jinsia na hata husababisha hali ya usawa.

Maswala ya ubaguzi, uana, utabaka na mielekeo ya utamaduni huletwa pamoja ili kuanzisha ufeministi unaomwangalia mwanamke kama kiumbe wala sio kwa msingi wa kijinsia. Ufeministi unachunguza utamaduni unaomlemaza mwanamke. Hili ni muhimu katika utafiti wetu ikizingatiwa kwamba katika tamaduni nyingi za Kiafrika dhana ya ukuu wa mwanamume dhidi ya mwanamke si swala geni.Dhana hizi za ubaguzi,uana na utabaka hazikuwepo katika utamaduni wa kiasili wa Kiafrika lakini ziliingia kupitia kwa athari za kikoloni na kibepari.

Mabepari walitoa mchango mkubwa kupitia kwa kazi ambazo zilitengewa wanaume na wanawake.

Mawazo mengine kuhusu ufeministi wa Kiafrika yanabainika katika maoni ya Wamitila (2003:253) kwamba,

> "Ufeministi ni istilahi inayotumiwa kueleza mojawapo ya nadharia ya uhakiki, imewekwa msingi na msukumo mkubwa, pamoja na nia ya kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kitamaduni, kidini, kijamii, kisiasa na kiuchumi. Ufeministi huishambulia mitazamo ya kiume kuhusu jinsi mwanamke anavyopaswa kuhisi, kufikiri na kuziitikia hali mbalimbali kimaisha".

Maoni haya ya Wamitila yanaonekana kukubali kwamba mwanamume ndiye kikwazo kikuu kwa ukombozi wa mwanamke.Wanawake wa Kiafrika nao wanapinga utamaduni unaomnyima mwanamke nafasi ya kutekeleza malengo yake. Kwa maoni yao, utamaduni unamfanya mwanamke kukosa uwezo wa kuchagua kuwa mke, kupashwa tohara na ukeketaji, kuwa kimya na hata kudhalilishwa hasa wale wanawake walio tasa.

Kwa ujumla, nadharia ya ufeministi inajaribu kuleta mabadiliko katika mitazamo ya kijinsia inayomkandamiza mwanamke na kutishia hali yake ya kijamii na kibinadamu. Tatizo la mwanamke litasuluhishwa tu iwapo haki na nafasi sawa itatolewa kwa wanawake kama ilivyo kwa wanaume. Kwa kuwa ufeministi wa Kiafrika una msingi katika thamani za Kiafrika na unazingatia masuala ya kijinsia yanayopatikana katika utamaduni wa jamii,unafaa kutumiwa kumkomboa mwanamke wa Kiafrika dhidi ya kukandamizwa kitamaduni,kidini,kisiasa na kiuchumi.Wanaanthropolojia kama Imbo (2002) aliyechunguza utamaduni wa Kiafrika anakubali kwamba kuna tamaduni zinazofaa katika jamii za Kiafrika.Tamaduni kama hizi

zinafaa kutumiwa ili kuendeleza matakwa ya wanawake.Maana ya mawazo hayo ni kuwa kuna mambo ya utamaduni yanayohusiana na wanawake na ambayo, yanaweza kutumiwa kumtengea mwanamke nafasi yake.

Katika kushughulikia nadharia ya ufeministi, ni bora ifahamike kwamba kuna baadhi ya mihimili ambayo ni ya kimsingi. Kwanza nadharia hii inatumia fasihi kama jukwaa la kuelezea hali ya mwanamke katika jamii. Nyimbo za taarab kama fani mojawapo ya fasihi simulizi ni mwafaka katika kuchunguza na kuelezea hali ya mwanamke katika jamii. Pili, nadharia hii inanuia kuleta usawa wa kijinsia na kitamaduni kupitia kwa miundo misingi inayopatikana katika jamii. Inapigania jamii mpya inayoheshimu jinsia ya kike kupitia kwa amali zake. Tatu, utafiti umeshughulikiwa kwa msingi wa kukisiwa kwamba mwanamke ametengewa nafasi ya chini katika jamii na hivyo basi mikakati kabambe lazima ibuniwe ili mwanamke aweze kutumia nafasi hiyo inayoonekana kuwa ni duni kusimama na kupigania nafasi yake. Mwisho, nadharia hii inalenga kuziweka wazi kazi za fasihi zilizotungwa na wanawake na ambazo zilipuuzwa kwa sababu ya utamaduni unaompendelea mwanamume.Utafiti huu umehakiki wimbo ulioimbwa na mwimbaji wa kike na wa kiume ili kuonyesha jinsi alivyoshughulikia swala la nafasi ya mwanamke. Kwa kuwa wanawake wa Kiafrika wanachukulia kwamba utamaduni ni njia ya kuleta uwiano wa kijamii, fasihi yao inadhihirisha hali hii ya unyonge kwa kuwa baadhi ya wanawake hawa wanakataa kujiita wafeministi.Utafiti huu umehakiki nyimbo mbili za taarab kimaudhui na kimtindo kwa minajili ya kuonyesha jinsi kila mmoja inavyomtetea mwanamke.

### 1.8.4 Msingi wa Uhakiki wa Kimtindo

Uhakiki wetu pia umeoongozwa na uhakiki wa  kimtindo.Uhakiki huu utafanywa kwa kuufuata mtazamo wa Leech (1969).

Wafula na Njogu (2007:97) wanasema kuwa, “kifasihi, mtindo huelezwa kwa kuainishwa na madhumuni ya msanii”.Kwa maoni yao madhumuni ni dhamira na mtindo ni jinsi dhamira zinavyowasilishwa.

Uhakiki wa kimtindo ulianza katika nchi za Kiyunani na Kirusi katika enzi za urasimi.Msisitizo katika uhakiki huu ulihusu jinsi ya kuzungumza,kupanga mjadala ,kutoa hotuba na kuwasilisha ujumbe.Moja kati ya masomo waliyofundishwa watoto ya Kiyunani ni jinsi ya kujieleza vyema.Wahakiki wa kimtindo walijihusisha na kutoa fafanuzi za matumizi ya lugha katika masimulizi,uteuzi wa maneno na mpangilio wake.Mawazo haya yanafaa kazi yetu kwa kuwa tunachunguza jinsi lugha inatumiwa kuendeleza maudhui katika fani ya nyimbo.

Kulingana na Njogu na Chimera (1999) wahakiki wa Urasimi wa Kirusi na Umuundo waliochangia ufanisi katika uhakiki wa kimtindo.Mwanamuundo anayesifika ni Roman Jakobson.Wanaendelea kusema kuwa kulingana na Jakobson ,fasihi ni matumizi ya nguvu dhidi ya lugha ya kawaida.

Mawazo haya ya uhakiki wa kimtindo kule Marekani na Uingereza yaliendelezwa na Leech (1969). Mwelekeo wa uhakiki wa mitindo uliendelea kubadilika na kuanza kuzingatia data nyingi zaidi ya kiisimu. Mabadiliko haya yalitokana na haja ya kuhusisha mwelekeo huu katika kuzichanganua fani nyingine za fasihi kama riwaya na tamthilia ndiposa wahakiki kama vile Leech (1969) na wengine wanaeleza matokeo ya mabadiliko haya kama mtindo mpya.Kulingana na maoni yao, mwelekeo huu mpya unazingatia mambo mengi na kusababisha hali ya utata.Utata huu unaleta ugumu wa kutoa tofauti kati ya njia za kueleza data na za kuchanganua

data hiyo.Katika kazi yake,Leech (1969:38-39) ameibuka na viwango vitatu vya lugha: “Utambuzi,mtindo na semantiki.” Katika kiwango cha kwanza cha utambuzi, ni lazima kwa msemaji kujua msamiati na sarufi lugha husika ili apate kuelewa jinsi ya kutunga sentensi.Msamiati na sarufi kwa pamoja huunda muundo rasmi wa lugha.Katika kiwango cha mtindo,fonolojia ya lugha hushughulikiwa.Sentensi huweza kuwasilishwa katika maandishi au mazungumzo. Kiwango cha tatu ni cha semantiki. Utafiti wetu umetumia tamathali za usemi katika kiwango cha semantiki. Kwa sababu semantiki inaeleza maana,maana itakayochukuliwa katika muktadha huu ni ya kikamusi.

Viwango vyote vitatu vya lugha hutumika katika uzungumzaji na usomaji na tofauti za viwango hivi hutokana na matumizi ya sheria za lugha kwa njia inayotofautiana.Leech (1969:38) anaongezea kwa kutoa mifano ya misemo yanayolingana katika kiwango fulani na vilevile kutofautiana katika kiwango kingine.Misemo hii ni kama vile:homofoni,uambishaji,sinonimi na polisemi.Mahusiano katika ngazi hizi hupatikana katika sentensi na kauli ndefu.

Wahakiki wa fasihi ya Kiswahili waliojishughulisha na uhakiki wa kimtindo ni pamoja na Kuhenga (1987) na Wamitila (2008).Kuhenga (1987) alishughulikia uainishaji wa tamathali za usemi na ufafanuzi wa dhana hizi.Kwa mujibu wa Kuhenga tamathali ni semi za mlinganisho wa tabia,za zinduna,za msisitizo,za kilinge,za mlinganisho wa mwigo na semi za maneno ya kutumbuiza.

Wamitila (2008) anasisitiza uainishaji wa tamathali za usemi kwa upana wake kwa kujumuisha tamathali za rasamu.Anaibuka na makundi manne ya tamathali ambazo ni:rasamu za

maneno,sentensi za sauti na za tafrika.Uainisho huu si wa ukiushi bali ni kwa kuafikiana na wahakiki wa fasihi ya Kimagharibi.

Kuna mambo mbalimbali ya kimsingi ya kuzihakiki kazi za fasihi kulingana na mitazamo ya kihakiki ya kimtindo.Katika utafiti wetu tutatumia uhakiki wa tamathali katika kuendeleza maudhui.Kwa kuwa tamathali za usemi zinapatikana katika lugha nyingi, wazungumzaji wengi hutumia mbinu hii bila kukusudia kwa kuwa ni mambo ya kawaida katika lugha.

## 1.9 Mbinu za Utafiti

### 1.9.1 Ukusanyaji wa Data

Utafiti ulifanywa makatabani na nyanjani.Sampuli yetu ilikuwa sampuli lengwa.Utafiti ulifanywa kwa njia zifuatazo; kwanza, uchunguzi wa kina ulifanywa kuhusu nadharia ya utafiti katika vitabu, majarida na machapisho mbalimbali katika maktaba. Tulikusanya data za kazi zinazojadili kuhusu nadharia ya ufeministi na uhakiki wa kimtindo. Pili, utafiti ulijumuisha kuzuru maeneo mbalimbali katika jiji la Nairobi, maeneo haya ni kama vile soko la Muthurwa, barabara za RiverRoad na Gaberone ambapo kuna maduka mbalimbali yanayouza kanda za video na tepurekoda za nyimbo za taarab ambazo zimerekodiwa katika maeneo mbalimbali na watunzi mbalimbali. Mbinu ya uteuzi wa data ni wa sampuli lengwa. Kwa kuwa nyimbo za taarab kama tulivyogundua katika ukusanyaji wa data ni chache mjini Nairobi, wapenzi wa nyimbo hizi ni wachache.Hali hii imesababisha kuwe na idadi ndogo ya wanaoendeleza biashara hii vivyo hivyo kuna idadi ndogo ya kanda hizi.

Baada ya kukusanya kanda za video na tepurekoda awamu iliyofuata ni kuzitazama na kusikiliza nyimbo hizi katika video na tepurekoda, uteuzi wa nyimbo mbili ulifanywa kwa kuzingatia mada ya utafiti.

Waimbaji, Mzee Yusuf na Mwanaidi Shaaban wanatoka katika bendi mbili tofauti nchini Tanzania, Mwanaidi na Afua wanaimba katika East Africa Melody naye Yusuf ni wa Jahazi Modern Taarab. Uteuzi wao ni kwa minajili ya kukidhi madhumuni ya utafiti wetu kwamba wanaume na wanawake wanaendeleza juhudi za kutetea nafasi ya mwanamke. Sababu nyingine ya kuteua Zanzibar ni kuwa ni kitovu cha nyimbo hizi katika pwani ya Afrika Mashariki baada ya kutolewa Misri. Tatu, nyimbo za taarab zilizo na umaarufu nchini zinatoka katika nchi ya Tanzania na zinachezwa katika runinga za humu nchini vilevile katika idhaa za redio kama QTV Citizen, KBC na zingine.

Mtafiti alikusanya kanda hizi na kisha akazisikiliza na kuzitazama kwa minajili ya kuteua zile zinazoshughulikia mada ya utafiti. Mapenzi ya mtafiti ya nyimbo hizi ilianza mwaka wa 1991 alipofundishwa nyimbo hizi na Makoti, aliyekuwa mwanafunzi wa Uzamifu katika chuo cha Moi.Kuanzia wakati huo mtafiti alipata hamu na stahamala ya kuzisikiliza na kunakili nyimbo hizi.

Njia ya mwisho ya ukusanyaji wa data ni kupitia kwa mtandao. Tumeyatafiti yaliyoshughulikiwa kuhusu mada kwa minajili ya kukusanya na kunakili mambo yaliyo na manufaa katika kazi yetu. Hatua ya mwisho katika utafiti ni kuzinakili nyimbo tulizokusanya kwa minajili ya kazi hii pia zile zilizotajwa na kuwekwa katika sehemu ya kiambatisho kama ithibati.

### 1.9.2 Uchanganuzi wa Data

Katika awamu hii ya uchanganuzi wa data, maswala ya kijumla yaliyobainika katika utafiti yalijadiliwa. Mbali na maswala haya ya kijumla maswala yanayozingira nyimbo kama ulivyo ushairi simulizi yalijadiliwa ili kuyatenga yanayohusishwa na nyimbo. Maswala haya ibuka yalijadiliwa katika sura za uchanganuzi.Data msingi ilichanganuliwa, na maelezo kutolewa kwa kuzingatia lugha na maudhui ya nafasi ya mwanamke (rejelea sura ya 2,3,4 na 5).

### 1.9.3 Umuhimu wa Utafiti

Ni matumaini yetu kwamba kupitia kwa utafiti wetu wa nyimbo za taarab, wahakiki wengine wa fasihi watapata ari ya kuweza kufanya uchunguzi zaidi wa nyimbo za taarab za kisasa kwa misingi ya nadharia mbalimbali za utafiti. Utafiti huu utawapa watafiti motisha wa kuyalinganisha na kulinganua maswala mbalimbali ya taarab ya zamani na ya sasa ili kubainisha tofauti zilizopo.

## 1.10 Hitimisho

Katika sura hii tulianza kwa kueleza kuhusu jamii ya Waswahili na athari za mtagusano wao na jamii zingine.Kisha tulieleza maana ya nyimbo za taarab kwa kurejelea mawazo ya wataalam mbalimbali wa fasihi pamoja na mchango wetu.Isitoshe tulieleza tatizo la utafiti na madhumuni kwa kujikita katika nadharia tete tulizoziteua.Pia tumeeleza sababu za kuchagua mada,kisha tukaeleza kuhusu upeo na mipaka ya utafiti.Tumezungumzia kuhusu msingi wa nadharia za utafiti,yaliyoandikwa kuhusu mada na mbinu za utafiti.Mbinu za utafiti zimegawanywa katika sehemu tatu:mbinu za ukusanyaji wa data,mbinu za uchanganuzi wa data na umuhimu wa data.

## SURA YA PILI:

## MAANA NA AINA ZA NYIMBO

### 2.0 Utangulizi

Katika sura ya kwanza tulichunguza maswala ya kimsingi yanayohusu utafiti wetu. Katika sura hii tunashughulikia aina za nyimbo na uamilifu wake katika jamii za Kiafrika.

### 2.1 Fani ya Wimbo

Wimbo ni fani muhimu ya fasihi simulizi katika jamii ya Waswahili kwa kuwa inatumika katika shughuli nyingi za kitamaduni. Shughuli hizi ni kama vile kazi, michezo, mapumziko na sherehe mbalimbali. Aidha, ni muhimu katika sherehe za kuzaliwa kwa mtoto, kupewa jina kwa mtoto, jando na unyago, na harusi. Kama tulivyobainisha baadaye, nyimbo za Waswahili hazitumiwi tu katika sherehe hizi kuburudisha bali hutekeleza majukumu mbalimbali ya kijamii. Majukumu yanayotekelezwa na nyimbo ni pamoja na kushauri, kuhimiza, kuliwaza na hata kusuta.

#### 2.1.1 Umbo na Mtindo wa Nyimbo

Nyimbo za Kiafrika haziimbwi huku waimbaji wakiwa tuli bali kuna utendaji. Utendaji huhusisha miondoko ya sehemu mbalimbali za mwili kama vile viuno, mikono, kichwa, miguu na kadhalika. Sehemu za mwili zinazotumika hutegemea utamaduni wa jamii husika. Katika jamii ya Waswahili, viuno, mikono na miguu ndizo sehemu zinazotumika sana katika utendaji.

Umbo la wimbo linajengwa na mistari ambayo wakati mwingine hurudiwarudiwa kutegemea malengo ya watendaji na huendelea hivi hadi kufika mwisho wa uimbaji. Sifa nyingine ya

mistari ni kuwa, kuna mistari inayoimbwa na watu mbalimbali lakini kuna mengine mahususi inayoimbwa na kiongozi ili aweze kudhibiti utendaji.

Swala la takriri katika mistari ya nyimbo za Kiafrika imefanyiwa uchunguzi na wasomi wa fasihi simulizi kama  Finnegan (1970).Anasisitiza kuwa matumizi ya mbinu hii ni nguzo muhimu katika nyimbo. Finnegan (1970:163) anaendelea kusema,

> "Kuna takriri nyingi katika ushairi wa Kiafrika. Mbali na kuwa una athari za kiujumi kuna thamani ya kimtindo ndani ya wimbo." (T.Y)

Yanayobainika katika kazi hii ni kuwa wimbo ni aina ya ushairi na una sifa sawa na sifa za ushairi kama ile ya takriri.Mfano wa matumizi ya takriri katika wimbo wa Kibiriti upele ni katika ubeti:

> *changanya changanya changanya*
> *kibiriti upele hunichanganyi naye*
> *funganya funganya funganya*
> *kibiriti upele hunifunganyi naye*

Sifa nyingine muhimu katika nyimbo za Waswahili ni kuwa, kuna uhuru wa kufaragua.Waimbaji hufaragua wimbo fulani ili kuufanya utumike katika muktadha au sherehe tofauti na ile iliyotungiwa. Nyimbo kama vile za kusuta huweza kufanyiwa ufaraguzi na kutumika katika muktadha mwingine tofauti.

Sifa nyingine ya wimbo ni waimbaji.Nyimbo huwasilishwa kwa njia ya mdomo na sauti ndiposa mwimbaji ni kiungo muhimu katika kuwasilisha ujumbe. Finnegan (1970) anasema kwamba

> "Kuwepo kwa fasihi hakuwezi kukamilika pasi na kuwepo kwa mwimbaji au mzungumzaji".(T.Y)

Katika baadhi ya nyimbo mwimbaji ni mtima wa wimbo kwa kuwa kupitia kwake ujumbe wa msanii hufikia hadhira.Mwimbaji anaweza kusitisha uimbaji ikifikia sehemu fulani na akaanza kuzungumza na hadhira au waimbaji wengine ili kupasha ujumbe kwa njia ya mazungumzo. Mfano kutoka katika wimbo wa *Tupendane Wabaya Waulizane,* ni kuwa mwimbaji anawauliza wachezaji wa ala wawachezee hadhira ala zao kwa kumtaja mmoja huku ala zikiendelea kuchezwa.Mfano, mwimbaji anasema, “Chimoi,wapigie Watanzania ngoma wausikize."

## 2.2 Maana ya Wimbo

Fafanuzi mbalimbali zimepata kutolewa kuhusu nyimbo, fafanuzi hizi hutolewa ili kukidhi mahitaji ya mtafiti. Kamusi ya Tuki (1981:463) inasema,

> “Wimbo ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya muziki.”

Ufafanuzi huu unasisitiza tu utamkaji kwa sauti ya muziki na unafaa kwa kazi yetu kwa sababu sisi tumejikita katika nyimbo za Kiafrika ambazo huimbwa kwa sauti ya muziki zikiambatanishwa na ala na pia kuna utendaji. Mulokozi (1981) anaeleza kwamba nyimbo ni kile kinachoimbwa. Anaendelea na kutoa sifa za nyimbo kama vile:

- Muziki wa sauti ya mwimbaji
- Muziki wa ala
- Matini au maneno yanayoimbwa
- Hadhira inayoimbiwa
- Muktadha wa uimbaji kama vile ibada, sherehe na kilio

Kwa maoni yetu, nyimbo za taarab zina sifa zote zilizotajwa hapa juu na kuwa ufafanuzi huu unafaa kutumiwa kuelezea maana ya nyimbo hizi.

Kwa kuwa nyimbo tofauti huwa na jumbe tofauti kwa hadhira mbalimbali, uimbaji hutegemea umri wa wanaoshiriki, jinsia, shughuli inayohusishwa na nyimbo na muktadha. Kulingana na Chesaina (1991:143) ,"nyimbo za dini miongoni mwa jamii ya wakalenjin huimbwa baada ya kipindi kirefu cha ukame ili kumwomba Mungu wao awajalie mvua".Anaongeza kuwa waimbaji wa nyimbo hizi ni wanawake wakiwa uchi nyakati za usiku.Mawazo haya yanaonyesha kwamba waimbaji ni wanawake na muktadha ni wakati wa janga la ukame.

Kama tulivyotanguliza sura hii kwamba nyimbo zina majukumu mbalimbali,tumetoa maelezo ya baadhi ya aina za nyimbo hizi na majukumu yao.

## 2.3 Aina na Dhima ya Nyimbo

Takriban, kila jamii za Kiafrika zilikuwa na nyimbo zilizo na maudhui kutegemea shughuli za kila siku kama vile; kazi, vita, maadili, malezi na mafanikio. Jamii ya waswahili ina aina mbalimbali za nyimbo ambazo hutumika katika sherehe mbalimbali za utamaduni wao. Nyimbo hizi ni kama vile lelemama, chakacha na taarab. Katika utafiti huu tumeshughulikia nyimbo za aina ya taarab.

Taarab kwa mujibu wa Askew (2002:102-3) ni,

> "Ni neno la Kiarabu lenye maana ya muziki unaopendeza na kuleta hisia za furaha,starehe na hata kuburudisha".(T.Y)

Ufafanuzi wa Askew kuhusu taarab huweza kuchukuliwa kuwa ni aina za nyimbo za kuburudisha. Ni kweli kuwa, kimsingi nyimbo hizi ziliwaburudisha masultani na wengineo lakini baadaye zilianza kutumika katika sherehe kama za harusi katika jamii ya Waswahili na ambapo pia zilitumika kuburudisha. Umaarufu wa nyimbo hizi uliongezeka kutokana na

mitagusano ya kijamii baina ya Waswahili na watu wa jamii zingine walioingia mwambao wa pwani ya Afrika Mashariki.

Watafiti wengi wa Kiafrika wanakubali kwamba nyimbo zina nafasi muhimu katika jamii kama anavyosema Wamitila (2003:107);

> "Takriban shughuli zote za binadamu kama kulima, kusuka, kuoa, kulea, kufariji, kuliwaza na kuzika, huandamana na nyimbo na uimbaji."

Nyimbo zinaweza kuimbiwa watu mashuhuri katika jamii ili kuwatumbuiza wakati wa mapumziko. Tafiti kuhusu taarab ya kale ilidhihirisha kuwa Sultani na wafanyibiashara mashuhuri walitumbuizwa katika kumbi maalum. Mmoja wa watafiti hawa ni Finnegan (1970) anasema kwamba,

> "Katika falme za kitamaduni za Afrika, baadhi ya watunzi na washairi walihusishwa na kumbi za watawala na walipokea zawadi kama wataalam."

Mawazo kama hayo yanaendelezwa na marehemu Bi.Kidude alipohojiwa katika gazeti la Nation (2013:DN2,2) .Alikiri kuwa alishiriki katika nyimbo za kumtumbuiza sultani kule Zanzibar katika miaka ya nyuma kabla ya uhuru wa Tanzania.

Kutokana na maelezo kuhusu nyimbo ni wazi kwamba kuna aina nyingi za nyimbo kulingana na majukumu yazo. Tumeangalia na kuzieleza baadhi ya aina za nyimbo zinazopatikana katika jamii za Kiafrika huku tukitolea mifano kutoka kwa baadhi ya beti za nyimbo za taarab za Waswahili. Nyimbo hizi ni kama vile; nyimbo za mapenzi, nyimbo za harusi, nyimbo za maadili, nyimbo za sifo na nyimbo za kusuta.

### 2.3.1 Nyimbo za Mapenzi

Hizi ni nyimbo ambazo huwasilishwa kwa ufundi ili kuonyesha hisia za furaha ama masikitiko.Hisia za furaha hutokea pale mwimbaji anapomsifu mpenzi wake au za kusikitisha ikiwa mwimbaji ni mtu aliyeachwa na mpenzi au anampenda mtu na huyo mtu hampendi. Utunzi wa nyimbo hizi kwa wakati mwingine hulenga kuwepo kwa usemezano fulani kati ya mwimbaji na anayelengwa. Wahusika huonyesha hisia zao kwa kutabasamu, kucheka na hata kutoa machozi ya huzuni au furaha tele.

Utafiti uliofanywa na Finnegan, katika jamii ya Wazulu ulidhihirisha kuwa mashairi ya mapenzi yalikaririwa na wanawake. Jambo hili linabainika katika jamii ya Waswahili ya Afrika Mashariki kupitia kwa nyimbo za taarab, hasa katika sherehe za harusi. Mfano wa ubeti mmoja wa wimbo wa *Tupendane Kwelikweli*, kudhihirisha hisia za kimapenzi:

*Tupendane kwelikweli wabaya waulizane,*
*Unijali nikujali vipembeni wanong'one,*
*Amebani makatili penzi letu wasilione*
*Liwaume penzi hili vipembeni wanong'one,*
*Liwaume penzi hili na dawa wasizione,*

Katika wimbo huu mwimbaji ambaye ni wa kiume anaelezea hisia za kimapenzi. Anamshauri mpenziwe waendelee na penzi lao na asikubali kusikiliza maneno ya mahasidi ambao daima wako mbioni kutaka kuwatenganisha. Aidha anawakashifu mahasidi na kuwajulisha kuwa hawatafaulu katika njama zao. Mwimbaji hapa amempa mwanamke himizo la kuamka na kutetea nafasi yake katika jamii kwa kupigania haki yake bila ya kukandamizwa na baadhi ya wanajamii.

### 2.3.2 Nyimbo za Harusi

Ndoa ni sherehe muhimu katika utamaduni wa jamii. Sherehe hizi huandamana na kila aina za tafrija ikiwemo nyimbo.Nyimbo hutumiwa kuwashauri wanaooana na hata kuwaelekeza kwenye matarajio na maisha yao ya unyumba. Nyimbo zingine huimbwa ili kuwasifu wazazi wa maarusi kwa malezi mema. Jamii ya msichana huhuzunika kwa kuondokewa kwa binti wao, huku ya mvulana ikifurahi.

### 2.3.3 Nyimbo za Maadili

Nyimbo hizi huimbwa kwa minajili ya kuwashauri wanajamii wawe na mienendo mema. Anayelengwa anashauriwa arekebishe mwenendo wake mbaya na kukumbushwa kuwa kuna aliye na nguvu (Mungu) na huweza kumpa kila mmoja riziki yake.Vilevile anakumbushwa kwamba yeye kama binadamu hana uwezo wa kuibadili hali yake ila akubali majaaliwa. Aidha, wanyonge wanashauriwa kujipa moyo kwa kuwa siku yao ya kuongoka itafika. Mfano wa wimbo wa maadili ni wa *Chuki Nichukie*, ulioimbwa na Leila, kifungu cha kwanza:

*Chuki si kizingiti cha kukosa ulichopewa,*
*Huandikiwi bahati we bure kunichukia,*
*Mola mgawa bahati na Mungu katupangia,*
*Tena huwa tofauti alopewa hupokea,*

Mwimbaji anawakashifu wale watu wanaoendeleza chuki kwa misingi ya kufanikiwa kwa wenzao kwa sababu ufanisi huo wa wenzao haukuwa kwa uwezo wao ila ni kwa kujaaliwa tu.

### 2.3.4 Nyimbo za Sifo

Nyimbo hizi huimbwa ili kumsifu shujaa fulani katika jamii. Huimbwa kwa kurudiwarudiwa kwa baadhi ya maneno ama sentensi ambazo zinalenga kumsifu anayerejelewa.

Takriri inanuia kumsifu anayelengwa kwa kumpa majina mbalimbali au hata kumsifu kwa vitendo vyake vya kishujaa. Sifa zinazotolewa zinaweza kuwa ni za jamii, koo au hata mtu binafsi. Mfano wa wimbo wa sifo unaomsifu mtu binafsi ni wa Isha Ramadhan, wa Mama Mashauzi.Ubeti moja katika ubeti huu ni:

*Unastahili pongezi kwa ulezi*
*Mama sio nguo mama sio kiatu*
*Wala mama sio mtandio*
*Na mwenzio sitaazima*
*Kwa yeye maskini mama*
*Tumboni mwake umekaa sana*
*Nimeapa sitoanza kumdharau mama.*

Wimbo huu unamsifia mwanamke kwa kumlea mwanawe na kwa kubeba mimba.Mama anaonyeshwa kama mtu muhimu na anafaa kuheshimiwa.

### 2.3.5 Nyimbo za Kusuta

Nyimbo hizi huimbwa kwa minajili ya kukejeli tabia fulani ambayo haipendezi na hata huweza kutumiwa ili kutoa mawaidha kwa njia ya tashtiti.

Nyimbo hizi zimechukua nafasi kubwa sana katika nyimbo za taarab. Wanawake hushambuliana hadharani hasa katika shughuli zao za kila siku kama vile kufua nguo. Wanawake wawili wanapokosana, kila mmoja atajaribu kutafiti na kujua mengi kuhusu hasimu wake mapema na kujitayarisha kumjibu kwa njia ya kukejeli.

Wanaoshambuliwa ni wale wanaoshukiwa kuwa wameshindwa kutekeleza majukumu yao ya unyumba ili wapate kurekebisha tabia zao. Mfano wa aina hii ya wimbo ni ubeti moja kutoka kwa *Nyaubati,* ulioimbwa na Fatuma:

*Nyaubati we umbea wauchorea ramani*
*Nyaubati kumba kumba wamkumbia nani?*
*Kutwa ni kwenye vijumba umgonganishe nani?*
*Umbea kwako ni shamba walima mazao gani?*
*Uchambue mshamba uwache sisi mjini*

Mwimbaji wa wimbo huu anazishambulia tabia za mwanamke kwa jina Nyaubati.Mwanamke huyu ana tabia ya kueneza uvumi na kuwagonganisha watu.Mwanamke anaonyeshwa kuwa ni mtu mvivu na kazi yake ni kuzurura ovyo ovyo badala ya kushughulikia jamii yake.

### 2.3.6 Nyimbo za Kizalendo/Kisiasa

Hizi ni nyimbo zinazoeneza ujitambuaji wa kijamii na huwaleta watu pamoja kama taifa.

Nyimbo hizi hulenga kuwashawishi watu kisiasa na kuwakosoa wanasiasa kwa matendo yao. Nyimbo za kitaifa ni mifano mizuri ya nyimbo za kizalendo. Nyimbo hizi zina dhima ya kusifu na kuonyesha hisia za kizalendo za nchi, utamaduni, au kikundi fulani. Aidha, huonyesha fahari katika utamaduni na mwelekeo wa taifa fulani. Nyimbo hizi huimbwa na watu wa jinsia ya kike na kiume.

### 2.3.7 Nyimbo za Jando na Unyago

Nyimbo hizi hutumiwa katika sherehe za kitamaduni, kama vile jando na unyago.

Katika jamii ya Waswahili, nyimbo hizi zilitumiwa kuwafundisha watoto wa kike mambo ya unyumba na unyago. Mawazo kama haya yanatolewa na marehemu Bi. Kidude kutoka Zanzibar (2013:2) kwamba ,

> "Niliwafundisha wanawake wachanga wa Waswahili kuhusu kubalehe, jinsi ya kuishi na waume zao na kupiga vita udhalilishaji wa kijinsia na kihadhi."(T.Y)

Mafunzo haya yalifanywa kupitia kwa mipigo ya ngoma za kitamaduni zikiambatanishwa na uchezaji wa ngoma.

### 2.3.8 Nyimbo za Dini

Hizi ni nyimbo zinazoimbwa ili kumsifu na kumtukuza Maulana kwa ajili ya uwezo alionao katika maisha ya binadamu. Kila mwanajamii anapenda kuhusishwa na uwezo huu mkuu. Nyimbo hizi huimbwa katika muktadha na sherehe za kidini kama vile ibada na kutoa kafara. Maulana alitunukiwa sifa tele. Mifano ya nyimbo za kidini katika jamii ya waswahili ni kama vile Kasida.

Mwenyezi Mungu hupewa sifa za kuwa na huruma, mnyenyekevu na mwenye uwezo wa kuumba. Aidha anawabariki watu na vitu mbalimbali na kwa hivyo binadamu anafaa kumheshimu.

## 2.4 Hitimisho

Kutokana na mifano tuliyoitoa ni dhahiri kwamba nyimbo zina nafasi muhimu katika jamii nyingi za Kiafrika na hutungwa ili ziafiki shughuli mbalimbali za jamii. Nyimbo za taarab zilitumiwa sana kuwatumbuiza wanajamii kwa muda mrefu sana, licha ya haya ujumbe unaowasilishwa una mafunzo mengi kwa wanajamii.

Jamii ya waswahili inaendelea kuthamini utendaji hai wa taarab katika jukwaa hasa katika sherehe za harusi na za kitamaduni hivyo kuongeza umaarufu wake nje ya jamii hii. Taarab japo imepitia mabadiliko mengi bado ingali imejidhibiti dhidi ya athari kutoka kwa mitindo mingine ya kigeni na kuibuka kama muziki wa Afrika Mashariki ulio na mtindo dhahiri unaoweza tu kulinganishwa na muziki wa bongo.

Kwa kuhitimisha, tumeziangazia aina chache za nyimbo kwa kulenga nyimbo za taarab ambazo tumezigawa kulingana na matumizi ya nyimbo hizi katika jamii. Japo tumeorodhesha na kuibainisha mifano michache haina maana kwamba nyimbo zote zimeshughulikiwa bali tuliona kuwa hizi zinafaa mada yetu ya utafiti na pia ni viwakilishi tosha vya aina za nyimbo zinazopatikana katika jamii za kiafrika. Uwanja wa nyimbo za taarab ni mpana na muda tulionao ni mfupi hatukuweza kuushughulikia uwanja wote.

## SURA YA TATU:

## MAUDHUI KATIKA KIBIRITI UPELE

### 3.0 Utangulizi

Katika sura ya pili mjadala ulifanywa kuhusu kuhusu aina mbalimbali za nyimbo,dhima na uamilifu.Mifano ya aina mbalimbali za nyimbo imetolewa kutoka kwa baadhi ya beti za nyimbo za taarab zilizokusanywa kwa lengo la kudhihirisha kwamba nyimbo za taarab kama zilivyo nyimbo zingine hutumiwa na jamii katika kutekeleza majukumu mbalimbali.

Sura hii inaendeleza mjadala kuhusu maudhui ya uteteaji wa nafasi ya mwanamke katika wimbo wa Kibiriti Upele kwa kuzingatia mawazo ya Millet (1969:157) kuwa, “inafaa kwa mabadiliko kamili yafanywe katika mifumo ya kijamii inayomkandamiza mwanamke”.(T.Y) Mabadiliko haya yanawezekana kupitia kwa mwanamke kujiimarisha kijamii na kiuchumi. Aidha tumechunguza nafasi ya mwanamke kama njia ya kuweka msingi wa uhakiki huo. Isitoshe dhuluma zinazomkabili mwanamke zimechunguzwa kama njia ya kuiwekea mada yetu ya nafasi ya mwanamke msingi imara.Tumeangazia dhuluma ili iweze kuwa kigezo muhimu cha kuhakiki nafasi ya mwanamke.Baadhi ya dhuluma zinazojitokeza katika uchunguzi wetu ni kubaguliwa kwa mwanamke katika ndoa, ukosefu wa mali na kuambukizwa kwa magonjwa. Pili, tumejadili harakati za kutetewa kwa nafasi ya mwanamke kiuchumi na kijamii na kubainisha jinsi zinavyoathiri nafasi ya mwanamke.

Wimbo wa *Kibiriti Upele(2009)* ulitungwa na Mahmoud El-Alawy na kuimbwa na Mwanaidi Shaaban ambaye ni mwimbaji katika bendi ya East African Melody nchini Zanzibar. Wimbo huu unahusu maisha ya ndoa katika jamii ya Kiafrika ya leo na inayokumbwa na misukosuko

mbalimbali. Kwanza kuna swala la uasherati na athari za ugonjwa wa ukimwi. Maswala haya mawili ndiyo yanayoelekeza mkondo wa maisha ya ndoa.

Wahusika katika wimbo huu ni watatu, wawili ni wa kike na mmoja ni wa kiume. Mhusika mmoja wa kike yaani ambaye ni msimulizi anakumbwa na msukosuko katika ndoa kutokana na tabia ya mumewe ya kuwa na mwanamke mwingine. Msimulizi anapinga tabia ya mumewe ya kuwa na mwanamke mwingine nje ya ndoa na anaishia kutengana naye. Mwanamume kwa upande mwingine anaambukizwa ugonjwa wa ukimwi na kubaki akiwa amesononeka baada ya kutengana na mkewe wa ndoa na kutorokwa na yule mwanamke aliyemfanya amsaliti mkewe.

## 3.1 Nafasi ya Mwanamke katika Ndoa

Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004:300) inasema kuwa ,“nafasi ni palipo patupu na ambapo panaweza kuwekwa kitu”. Ufafanuzi huu ukiwekwa katika muktadha wa kijamii una maana kwamba kila mmoja ana mahali pake alipotengewa na jamii ili apate kushiriki katika mambo ya kijamii. Nafasi ya mwanamke inahusu juhudi za mwanamke za kupinga ukandamizaji anaotendewa na mwanamume. Ukandamizaji huu ni pamoja na kunyimwa haki za kijamii na kiuchumi.

Mwanamke anaweza kujinasua kutoka kwa hali hii ya kukosa nafasi yake kwa kupinga utamaduni usiomruhusu kujitengea nafasi ya kutoa sauti yake. Aidha mwanamke anapaswa kutetewa kupitia kwa tamaduni zinazompa uhuru wa kufanya maamuzi kuhusu maisha yake. Haki za kumiliki mali na uamuzi wa mambo kama vile kuwa na mke mwenza, ni miongoni mwa maswala muhimu ambayo yangefaa kuwachiwa mwanamke ili apate kujiamulia mwenyewe.Katika wimbo wa kibiriti upele mwanamke anakumbwa na tatizo la uasherati kutoka

kwa mumewe.Mwanamume huyu ana mwanamke mwingine lakini hayuko tayari kumwacha hata baada ya kutishiwa na mkewe kwamba hayuko tayari kuishi naye.Mwanamume amejiamulia mwenyewe kuhusu maisha yake na hampi mwanamke nafasi ya kuamua iwapo ataishi katika ndoa ya aina hii au la. Aidha mwanamume ndiye mmiliki wa mali na anamwacha mwanamke kama mtegemezi.Yule mwanamke wa nje ya ndoa anakubali tabia ya uasherati na mume wa mwingine kwa sababu ya kukosa kujikimu kifedha.

**3.2 Dhuluma za Mwanamke katika Ndoa**

Ndoa ni asasi muhimu katika jamii yoyote ile; kwanza kwa kuwa ni msingi wa uzazi unaoendelezwa kupitia kwa watoto ingawa haina maana kwamba hakuna ndoa isiyokuwa na watoto. Pili uhusiano wa mambo ya ngono hukubaliwa katika ndoa. Jamii za Kiafrika zimempa mwanamume mamlaka katika ndoa na maamuzi ya maswala yote yanayohusiana na ndoa ni jukumu lake. Mwanamke kwa upande mwingine, inadaiwa kuhesabiwa kama mali ya mume miongoni mwa jamii za Kiafrika na hakuruhusiwa kuuliza wala kutekeleza majukumu aliyotengewa mwanamume. Matokeo ni mwanamke aliyedhulumiwa kimwili na kimawazo na aliyekubali hali yake duni.

Mwanamke katika jamii za Kiafrika amenyimwa nafasi yake katika ndoa kwa kukandamizwa na mwanamume, mwanamke hana sauti kuhusu masuala ya ndoa kama vile uchumba, mapenzi na uchumi. Mwanamume katika jamii ya Waswahili ana uhuru wa kuoa mke mmoja au zaidi kutegemea uwezo wake wa kiuchumi. Mwanamke kwa upande mwingine anatarajiwa avumilie katika ndoa ya aina hii ili isije ikasambaratika kwani kwa kufanya hivyo angesimangwa na hata kutengwa na wanajamii. Mwanamke katika ndoa hukumbwa na shida ambazo tumebaini hapa chini.

### 3.2.1 Uasherati

Baada ya harusi kufanyika, jamii hutarajia kuwa kutakuwa na heshima baina ya wanaohusika hasa kuhusu maadili ya ndoa. Lakini la kustaajabisha ni kuwa baadhi ya watu hawana uaminifu katika ndoa na sababu mbalimbali hutolewa kuhusu hali hii. Watu husema kwamba hali ya uasherati hutokea sana miongoni mwa watu wa tabaka la juu ambao wana mali ya kutosha na huweza kuzitumia kwa njia ya kuwadanganya wasichana na mabibi za wenzao. Wanawake pia hushiriki uasherati wakiwa na nia ya kufaidika kiuchumi kutoka kwa wanaume wengine. Mwanaidi ameyaonyesha haya katika mstari:

*Swali lake yeye huyo una hela huna?*

Mwimbaji anaishauri hadhira pamoja na jamii wajiepushe na mienendo kama hiyo.

Mwanaidi, katika wimbo wa *Kibiriti Upele*, anaonyesha maswala ya kibinafsi ya mwanamke kwa njia ya moja kwa moja na uwazi. Anaonyesha hisia zinazompata mwanamke pindi mume wake anapomwambia kwamba amempata mke mwingine, hisia za uchungu kutokana na usaliti zinadhihirika:

*Kama sababu ni huyo,*
*Akuzuzuaye huyo,*
*Kibiriti upele huyo,*
*Isikupe taabu basi isikupe,*
*Nenda naye basi nenda naye.*

Mwanamke katika kifungu hiki anasimulia hali yake ya kukerwa na tabia ya mwanamume iliyoruhusiwa na utamaduni; tabia ya kuwa na zaidi ya mwanamke mmoja. Hisia za kukereka za mwanamke zinadhihirika katika mstari wa nne, ***nenda naye basi nenda naye.*** Mwanamke huyu amechoshwa na tabia ya mume na yuko tayari kumwachilia kwani hamtaki tena. Anamfukuzia mumewe mbali kutoka kwake.

Hisia za kukereka zinaonekana katika maneno aliyoyatumia msemaji. Kumfukuzia mbali mume huyu kunatokana na hali ya uasherati. Mstari kibiriti upele unadhihirisha kwamba kuna mwanamke muasherati ambaye yuko tayari kuingilia kati ndoa ya msimulizi na mume. Mwanamke anayerejelewa kwa jina la *Kibiriti Upele* ni tishio kwa ndoa hii.

### 3.2.2 Usaliti

Usaliti ni shida nyingine inayomkabili mwanamke katika ndoa. Ufafanuzi wa kamusi wa usaliti ni tendo la kutoa siri. Katika muktadha huu tumechukulia usaliti kwa maana ya mwanamke kutendewa mambo kinyume na matarajio yake. Mume wa msimulizi amemchukua mke mwingine wa nje na kukosa kuiheshimu ndoa yake. Jambo hili ni la kuudhi sana na linamfanya msimulizi kuvunja ndoa yake. Usaliti kwa hakika hutokea miongoni mwa wanajamii. Ingawa huweza kutokea kwa njia tofauti huibua hisia za uchungu kama yanayobainika katika matamshi ya mwanamke kwamba:

*Usinitilie nuksi mimi nawe sina haja*.

Hisia za uchungu zinazotokana na usaliti katika wimbo huvuta hisia za hadhira.

## 3.3. Dhuluma za Kiuchumi

Mwanamke katika jamii nyingi za Kiafrika hakuruhusiwa kurithi wala kumiliki mali yoyote bali alikuwa chini ya mwanamume, hali hii imemfanya avumilie mateso mengi ili apate kujikimu. Wengine walitumia njia isiyo halali kama vile uasherati, utumizi wa dawa za kuwadhibiti wanaume na hata wengine kuishia kuwasababishia vifo waume zao katika harakati za kuwafanya kuwakimu. Katika mstari:

> *Swali lake yeye huyo huna pesa huna?*

Mwanamke anayerejelewa na msimulizi ni mnyonge na yuko radhi kumtegemea mwanamume kwa hali zote hata ikiwa ni kuvunja ndoa ya mwanamke mwingine.

Uadilifu wa mwanamke huyu pia unatiliwa shaka kwa sababu anashiriki ngono na vijana wa umri mdogo bora apate pesa.

### 3.4 Harakati za Kutetea Nafasi ya Mwanamke

Harakati hizi zinahusu juhudi za mwanamke za kujikomboa kutokana na ukandamizaji unaoendelezwa na mwanamume. Harakati hizi ni za kumpa mwanamke nafasi katika ndoa na mambo ya kiuchumi.

Mwanaidi katika wimbo wa *Kibiriti Upele* amemchora mwanamke kama kiumbe mwenye uwezo wa kupigania nafasi yake licha ya kupitia changamoto chungu nzima. Mwanamke haheshimiwi wala mashauri yake hayazingatiwi na jamii ya ubabedume.Mwanamume anakuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanamke wa nje.Licha ya kukanywa na mkewe anaendelea na tabia hii.Mwanamume huyu anawachwa na mkewe na anaambukizwa ugonjwa wa ukimwi.Mwanamke huyu anafaulu hatimaye kujinusuru kutoka katika hatari ya ugonjwa wa ukimwi hivyo,ametetea nafasi yake licha ya changamoto.

#### 3.4.1 Talaka

Hii ni hali ya mtu kutoka katika ndoa baada ya kutengana na mwenzake. Mwimbaji ametumia mbinu hii ili kumpa mwanamke nafasi yake.

Katika kifungu:

*Kama sababu ni huyo,*
*Akuzuzuaye huyo,*

*Kibiriti upele huyo,*
*Isikupe taabu basi isikupe,*
*Nenda naye basi nenda naye,*

Msimulizi ambaye ni mwanamke, anatetea nafasi yake. Kwanza anamkejeli mumewe kwa kujihusisha na uasherati na mwanamke anayemwita kwa jina ***Kibiriti Upele*** linalomaanisha anayetangatanga. Pili, mwanamke yuko tayari kutengana na mumewe mwenye tabia ya uasherati ndiposa anamwambia ana uhuru wa kwenda kwa yule *Kibiriti Upele* kwa kusema, ***nenda naye basi naye***.

### 3.4.2 Uerevu na Umakinifu

Uerevu na umakinifu ni sifa nyingine anazomiliki mwanamke katika wimbo wa *Kibiriti Upele*. Mwanamke ameonyeshwa kugundua azma ya yule mwanamke muasherati. Anamtahadharisha mumewe dhidi ya kuchezea maisha yake kwa kuwa na uhusiano na wanawake wengine nje ya ndoa. Isitoshe mwanamke hayuko tayari kukubali kuwa na mke mwenza kwa sababu tabia kama hii ina madhara yake. Kifungu kinachofuata kinarejelea hali inayojadiliwa:

*Hujipendi najipenda hujitaki najitaka,*
*Pendo la shirika ninaliogopa,*
*Changanya changanya changanya,*
*Kibiriti upele hunichanganyi naye.*

Mwanamke katika kifungu hiki amechorwa kama mwenye uadilifu na jasiri kinyume na mwanamume. Vilevile nafasi yake katika ndoa inabainika; mwanamke ananena na mumewe kwa ujasiri na kumwonya dhidi ya utamaduni potovu wa uke wenza na hata kutishia kumwacha ikiwa ataendelea na tabia kama hii.

Mhusika ambaye malalamishi yanatolewa juu yake amechorwa kama asiye adilifu kwa kuendeleza uasherati na vijana wadogo bila hata ya kujali umri:

*Kamfate hana choyo wala ye muhali hana,*
*Kamfate ana moyo muhimu kwake pa jina,*
*Maarufu kifyagio yeye jamvi la vijana,*

Matumizi ya maneno **kifyagio** na **jamvi la vijana** ni sitiari za uchafu wa mwanamke anayejihusisha na uasherati. Jamvi la vijana ni aina ya mkeka unaotumiwa na vijana kukalia, maana ni kuwa mwanamke anayerejelewa anachezewa na vijana katika uasherati na vijana wenyewe ni wa umri mdogo. Kifagio ni chombo cha kutoa uchafu na huwa kichafu. Sitiari hii ya kifagio ni ishara ya uasherati.

### 3.4.3 Uadilifu

Katika juhudi za kumtetea mwanamke, mwimbaji amebainisha madhara yanayoweza kutokea katika jamii baada ya kuyapuuza mawaidha ya mwanamke. Mwanamume anayerejelewa katika wimbo anaambukizwa ugonjwa wa Ukimwi, ndoa imesambaratika na mwanamume anaachwa katika upweke. Mwanamume katika kifungu cha hapa chini anaonyeshwa kama muasherati, asiye na uadilifu na asiyeyathamini mawaidha ya mwanamke lakini mwanamke ni adilifu. Adili katika Kamusi Sanifu la Kiswahili (2008:5) ni tendo la wema. Maelezo mengine ambayo yamepata kutolewa kuhusu maadili ni kwamba vitendo vya uadilifu ni vile vinavyoleta raha kwa watu wengi. Mwimbaji anachangia swala la uadilifu katika kifungu:

*Basi usijipe taabu wewe basi,*
*Basi sikutaki tena wewe basi,*
*Basi nenda naye huyo wewe basi,*
*Kufa rwako hufi nami kufa rwako.*

Msimulizi, katika kifungu hiki anamjulisha mumewe kuwa hawezi kuishi naye kwa sababu ana mke mwingine. Anaendelea na kumtahadharisha mumewe kwamba akiendelea na kuwa na uhusiano na mke muasherati mwishowe atakuja kufa. Hatima ya vitendo vyake ni kuambukizwa ugonjwa. Ili kujiepusha na maafa haya mwimbaji anatupa ushauri katika kifungu:

*Kama kweli wanitaka,*
*Nenda kapimwe ukimwi,*
*Na uwache mseto,*

Mwimbaji anatueleza kwamba watu hujaribu kutekeleza mambo mengine maishani na yasiyofaulu na kuishia kujilaumu. Madhara yanayoweza kumpata mtu kutokana na kukosa kuzingatia mawaidha yameonyeshwa katika kifungu:

*Mwoneni huyo mwoneni huyo,*
*Amekuwa hafungani amejishusha taabani,*
*Apitapita njiani amekosa na imani,*
*Amekuwa hajioni siye tena wa zamani,*

Maneno, ***mwoneni huyo mwoneni huyo***, ni ya kumdhihaki mwanamume. Mwanamume huyu alikataa kufuata mashauri ya mkewe ya kuacha kuwa katika uhusiano wa kimapenzi na mwanamke mwingine na kujipima ili apate kujua ikiwa ana ugonjwa wa ukimwi au la. Maneno katika mstari huu yamekaririwa kuambatana na azma ya mwimbaji ya kutaka kusisitiza kwa jamii ione jinsi madhara ya ugonjwa wa ukimwi yanavyoweza kumpata yeyote.

Mwanamke anaonekana mwerevu na mwangalifu sana na kila wakati kunapotokea tishio huwa katika mstari wa mbele katika kung’amua hatari na kisha hutahadharisha jamii dhidi yake. Mwanamke hutafuta mbinu mbalimbali za kujaribu kukinga jamii dhidi ya maangamizi.

Mwanamke ameweza kutetea nafasi yake katika ndoa kwa kumtaliki mumewe na anaepuka kuambukizwa ugonjwa wa ukimwi na kuonekana akimkejeli huyu mume kwa maneno haya.

Ukimwi ni ugonjwa wa kuambukizana kupitia kwa ngono; ugonjwa huu ni sitiari ya maisha ya sasa yaliyo na changamoto nyingi na unatumiwa kuwaonya wanajamii dhidi ya kuendeleza tamaduni potofu zinazoweza kudhuru maisha ya binadamu. Utamaduni wa kuwa na wake wengi umepitwa na wakati ndiposa mwimbaji amemwonyesha mwanamke adilifu akiepuka ugonjwa wa ukimwi.

Mwanamke katika wimbo huu amegundua hatari ya ugonjwa wa ukimwi na anamtahadharisha mumewe na mwenyewe kuchukuwa hatua ya kujikinga mapema, matokeo ni kuwa ugonjwa wa ukimwi haumpati.

*Kama kweli wanitaka kama kweli wanitaka,*
*Nenda kapimwe Ukimwi,*
*Na uwache mseto na uwache mseto,*

Katika mstari wa tatu suluhisho linatolewa na mwimbaji kuhusu kujikinga dhidi ya kuambukizwa ugonjwa wa ukimwi ni kwa kuepuka uasherati na uke wenza. Pia wanajamii wanashauriwa kujipima kabla ya kuoana ili wajue iwapo wameambukizwa.

Uwasilishaji wa ujumbe kwa njia iliyo wazi na mwanamke wa kisasa unabainika. Mwimbaji anataja ugonjwa wa ukimwi hadharani na njia ya kujikinga na kuonyesha kuwa haya si mambo ya kufichwa.

*Kama kweli wanitaka nenda kapimwe ukimwi*

Kwa kutumia mwanamke kama sauti yake, mwimbaji anaonyesha kwamba kwa kuwashirikisha wanawake katika maamuzi ya kijamii kwa hakika maendeleo yatapatikana.

**3.5 Nafasi ya Kiuchumi**

Mwanamke anafaa asimame na kupinga ukandamizaji wa kiuchumi. Millet (1969:157) kwa kuendeleza maoni ya mwanamke kujikomboa kiuchumi anahimiza,

> “Kuwe na mabadiliko kamili katika mifumo ya kijamii inayomkandamiza mwanamke.”(T.Y)

Mabadiliko haya yanawezekana tu kupitia kujiimarisha kwa mwanamke kijamii na kiuchumi. Mwanaidi amempa mwanamke nguvu ya kuweza kupigania nafasi hii ya kiuchumi kwa kumhimiza kukataa kuishi na mwanamume muasherati eti kwa sababu ana fedha.

*Mzito hakufahamu mimi naye sina hamu,*
*Amtakaye amchukue mchukue mchukue mchukue*.

Anayerejelewa hamtaki tena mume muasherati na aliyeambukizwa ugonjwa wa ukimwi. Mwimbaji ameonyesha kwamba mwanamke ni jasiri na mwangalifu, kwanza kwa kugundua madhara ya uasherati kwa kujiepusha nao. Pili anavunja ndoa isiyokuwa na uaminifu na yu tayari kuendelea na maisha yake bila ya mume, kinyume na yule kibiriti upele ambaye anahatarisha maisha yake kwa sababu ya fedha. Aidha mwanamke amejikomboa kimawazo kwa kukataa utamaduni unaomruhusu mwanamume kuwa na zaidi ya mke mmoja na mwanamume kuwa tegemeo la mwanamke.Anasema;,

*Pendo la shirika ninaliogopa,*
*Kibiriti upele hunichanganyi naye,*

Kibiriti upele kama tulivyosema ni sitiari ya mwanamke muasherati. Mwanamke huyu anakataliwa na msimulizi kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mume wake wake kwa sababu msimulizi anafahamu madhara yanayotokana na mahusiano kama hayo.

Aidha anaelewa thamani ya maisha yake kinyume na mumewe, anaposema:

*Hujipendi najipenda hujitaki najitaka***.**

### 3.6 Hitimisho

Asasi muhimu zinazochangia kudunishwa au kumkomboa mwanamke zilibainika kuwa ni ndoa na uchumi. Mawazo kwamba mwanamke anachorwa kama kiumbe duni hayana mashiko yoyote katika data yetu kwa sababu juhudi zinafanywa na waimbaji kumtetea mwanamke kwa kumpa mbinu za kutetea nafasi yake. Mwelekeo chanya wa jamii kuhusu mwanamke unabainika katika maudhui ya wimbo huu. Kwa kufanya hivi nyimbo husaidia katika kuendeleza juhudi za kumtetea mwanamke dhidi ya ukandamizaji kama tulivyoona katika sura hii.

Ingawa wimbo huu wa *Kibiriti Upele* hautaji jinsia ya anayerejelewa tunaweza kukisia tu kuwa ni mwanamke kwa sababu mwimbaji ni mwanamke na husemekana kwamba mwimbaji anaweza kuwa anawasilisha hali yake na kuonekana kama anawasilisha matukio ya jamii.

## SURA YA NNE:

## MAUDHUI KATIKA TUPENDANE WABAYA WAULIZANE

### 4.0 Utangulizi

Katika sura ya tatu tumeweza kujadili kuhusu nafasi ya mwanamke na kudhihirisha jinsi asasi ya ndoa inavyoendeleza hali hii. Aidha tumebainisha jinsi mwimbaji wa nyimbo ya *Kibiriti upele* alivyojaribu kutetea nafasi hii ya mwanamke.

Sura hii ya nne inaendelea kuonyesha jinsi mwimbaji Yusuf, anavyoshughulikia swala hili la nafasi ya mwanamke katika wimbo wa *Tupendane Wabaya Waulizane*. Kama tulivyotanguliza katika sura ya tatu wimbo huu uliimbwa na Yusuf katika bendi ya Jahazi Modern Taarab. Wimbo huu unasimulia kuhusu majukumu ya mwanamke katika maisha ya ndoa. Kwa kuwa ndoa haiwezi kufanyika nje ya jamii, wanajamii wanaonyeshwa kuuathiri uhusiano wa wanaohusika.

Hapo kale uteuzi wa uchumba ulitegemea tabia, wajihi na familia. Ikiwa familia fulani ilisifika kwa mambo maovu kama vile uchawi au kuwa na historia ya ugonjwa fulani, watu walichelea kuoa katika familia hiyo. Siku hizi uteuzi wa uchumba hupimwa kwa kigezo cha mapenzi,mali na sifa. Hali hii imebadilisha malengo ya ndoa na kuyafanya kuwa ya mapenzi, kujitajirisha na kujihusisha na ukoo maarufu. Katika wimbo unaorejelewa,mwimbaji anaishauri jamii kujiepusha na ndoa ambayo haijajengwa kwa misingi ya mapenzi, kwa sababu ndoa kama hizi huenda zikavunjika. Mwimbaji anazungumzia hali hii katika wimbo wa *Tupendane Wabaya Waulizane.*

Yusuf ameanza wimbo wake kwa kutaja jina la Maulana.Hii inaashiria kwamba binadamu hana uwezo wowote kuhusu maswala kama vile ndoa na mahusiano katika jamii.Yanayofanyika katika jamii ni majaaliwa:

*Siku zote wa kuombwa ni Mungu,*
*Yetu sote alopanga ni Mungu,*

Katika jamii kuna watu ambao huonea wenzao wivu sana waonapo ndoa za wenzao zikifaulu. Watu kama hawa hujaribu kutafuta njia za kuwatenganisha wenzao. Wanaweza kuzua uwongo ili wasababishe mizozano.Swala la wivu linaonekana katika wimbo huu ndiposa mwimbaji anawaonya walio katika ndoa wasiyasikilize maoni ya watu kama hawa wala wasiwape nafasi ya kuwatenganisha. Mawazo haya yanabainika katika kifungu:

*Hawa maadui zetu wanafanya kila hila,*
*Na hili penzi letu linalindwa na Mola,*
*Hatuwapi nafasi tunawapa tuendesha,*
*Hawa wapambe nuksi jeuri tutawaonyesha,*

Mwimbaji ambaye ni wa kiume anatumia maneno haya ili kumwonya mwanamke dhidi ya kuwasikiliza wanajamii wenye nia mbaya kwa ndoa yao.

**4.1 Mapenzi**

Wimbo huu unazungumza kuhusu swala la mapenzi katika ndoa. Swala hili linaweza kudumishwa tu ikiwa wanaohusika watashirikiana na kukataa kuingiliwa na jamii. Mume na mke wanashirikiana kudhibiti ndoa yao. Suala hili linajitokeza katika wimbo huu katika mistari:

*Tupendane kwelikweli wabaya waulizane,*
*Unijali nikujali vipembeni wanong'one,*

### 4.2 Majukumu ya Mwanamke

Mwanamke kama mlezi wa jamii anachangia katika kudumisha mahusiano. Mwimbaji amempa mwanamke ushauri kuhusu njia za kutumia ili kumdhibiti mwanamume. Njia hizi ni kama vile mapishi, maongezi na malezi.

#### 4.2.1 Mapishi

Ni wajibu wa mwanamke kukidhia mahitaji ya mume ya chakula kutokana na ujuzi wa upishi. Vyakula vilivyotajwa ni pamoja na chai ya tangawizi na juisi ya parachichi. Vyakula hivi vinahitaji ujuzi ili kuvitayarisha na mwanamke ambaye atayafanya haya humteka bakunja mwanamume. Mwimbaji anampa ushauri huu mwanamke ili ajitengee nafasi yake. Mfano katika mistari,

*Honey basi nipe chai yenye nyingi tangawizi,*
*Kisha unitayarishie juisi ya parachichi,*

#### 4.2.2 Maongezi

Maneno ni mbinu ambayo jamii hutumia katika kuwasilisha ujumbe na hisia mbalimbali. Hisia hizi huweza kuwa za furaha, uchungu na hasira. Mwimbaji anamshauri mwanamke atumie lugha tamu kwa mumewe ili wadumishe mapenzi yao;

*Sweety usiku unibembeleze uje mwema usingizi,*
*Sweety nikiwa hoi wayaja na makamusi,*

#### 4.2.3 Malezi

Mwanamke ndiye chemichemi ya maisha. Ndiye mlezi wa  watoto; ndiye humwongoza mtoto maishani mwake. Mwanamume katika wimbo huu anatunzwa kama mtoto. Mwimbaji anatumia hali hii ya malezi ya mume katika kuchora picha ya mwanamume kama kiumbe dhaifu na

ambaye anahitaji kutunzwa kwa uangalifu. Kwa upande mwingine, umuhimu wa mwanamke kama mlezi hauwezi kupuuzwa. Mistari ifuatayo inaonyesha dhana hii ya malezi:

*Honey nataka unibebe unipeleke kuoga,*
*Sweety nilishe nishibe hata mlo uso mboga,*
*Sweeti usiku unibembeleze uje mwema usingizi,*
*Honey taratibu unilaze tukutane kwenye njozi,*

Mwanamke anamlea mwanamume kwa kumwosha, kumlisha, kumbembeleza na kumlaza kama mtoto. Hili linaashiria kuwa mwanamume anamtegemea mwanamke kwa mahitaji yake yote ya kibinadamu na bila ya mwanamke maisha yake yangekuwa magumu. Uhusiano wa mwanamke na mwanamume katika swala la ngono limeangaziwa na mwimbaji. Mwanamke ndiye aliye na nafasi kubwa kwa kuwa anaweza kutumia mbinu hii ili kumdhibiti mwanamume. Haya yanabainika katika kifungu;

*Kisha unipe kila kitu tulichohalalishiwa,*
*Nami nikupe mavitu we mwenyewe unanijua,*
*Kisha tucheze sebende letu mpaka joto analia,*
*Kwa kila mmoja wetu wakituona tazimia,*

Kumpa kila kitu kilichohalalishiwa ndiyo tendo la ngono. Tendo hili hukubaliwa kutendeka katika ndoa kulingana na desturi za dini ili kuendeleza uzazi.

Mwimbaji anatamatisha wimbo kwa kutoa hisia zake za kumpenda mpenziwe na kuahidi kwamba hatamwacha. Aidha umuhimu wa Maulana unatiliwa mkazo. Maulana ana uwezo wa kuwaadhibu wale wanaoingilia ndoa za watu:

*Nuru imetuwakia tunamshukuru Mungu,*
*Wale waliotupangia na kutuletea majungu,*
*Mungu atawaunguza kwa miiba ya sungu,*

**4.3 Hitimisho**

Katika wimbo huu maswala ya kawaida ya uhusiano wa wanawake na wanaume katika ndoa yameshughulikiwa.Mwimbaji ameonyesha kuwa mwanamke ana nafasi muhimu katika mahusiano hayo.Aidha mwimbaji amempa mwanamke mbinu za kutetea nafasi yake katika ndoa. Mbinu hizo ni zile zinazopatikana katika mazingira ya mwanamke kulingana na nafasi alizotengewa na jamii.Mazingira hayo ni ya nyumbani.Kama inavyofahamika ni kuwa katika jamii ya Waswahili, mwanamke anatarajiwa kufanya kazi za nyumbani huku mwanamume akizifanya za nje ili kila mmoja ashiriki katika kukidhi mahitaji ya jamii.

Mbinu ambazo mwimbaji amempa mwanamke ili atetee nafasi yake ni kama vile kumtunza mumewe vizuri, kupika, kumfurahisa kwa maneno na kumpa mapenzi.Akiyafanya haya kwa hakika atakuwa amepata fursa ya kutetea nafasi yake.

## SURA YA TANO:

MATUMIZI YA LUGHA KATIKA KIBIRITI UPELE NA TUPENDANE WABAYA WAULIZANE

### 5.0 Utangulizi

Sura ya nne imeendeleza swala la maudhui katika wimbo wa Tupendane Wabaya Waulizane.Tumeweza kuonyesha jinsi mwanamke anaweza kutumia nafasi aliyotengewa na jamii kutetea hali yake duni.

Katika sura hii tumebainisha jinsi lugha ilivyo muhimu katika kuonyesha mwelekeo wa jamii kuhusu nafasi ya mwanamke. Aidha tumejadili jinsi lugha inavyoweza kutumiwa kubadilisha mwelekeo uliopo wa jamii kuhusu mwanamke kwa manufaa ya mwanamke mwenyewe. Uchanganuzi huu wa lugha umefanywa kwa lengo la kuonyesha jinsi lugha imetumiwa kuelezea maudhui ya waimbaji wa nyimbo mbili za taarab**.**

### 5.1 Taarab ya Kisasa

Mwanaidi Shaaban na Mzee Yusuf ni waimbaji wa taarab wanaosifika. Aina ya taarab inayoendelezwa na waimbaji hawa ni ile inayoitwa taarab ya kisasa.Aina hii ya taarab ni tofauti na taarab ya kale kimtindo; lugha inayotumiwa na utendaji ni tofauti. Mtindo wa kisasa unadaiwa kuwa umekiuka maadili kupitia kwa miondoko iliyo hasi na ya kasi; aidha lugha inayotumiwa haina heshima (lugha ya kero na chukizi). Kinyume na taarab ya kale, iliyokuwa na sifa za ushairi wa kidhahania wenye ujumbe uliofichika na utendaji wake wa utaratibu.Mawazo haya ya uwazi wa taarab ya kisasa yanapatikana katika mtandao wa tovuti, katika mawazo ya Mohamed (2009), mwimbaji na mwanzilishi wa kikundi cha wanamuziki wa taarab cha East Afrika Melody nchini Tanzania.

Anaripotiwa katika gazeti moja humu nchini akisema kwamba maneno ya taarab ya kikale yana maana fiche.Anaendelea kusema kuwa watunzi walitumia jazanda katika nyimbo nyingi bila kukusudia.Mawazo haya yanaoonyesha kuwa matumizi ya jazanda lilikuwa ni jambo la kawaida nyakati hizo.Ufumbuaji wa maana uliwachiwa msikilizaji katika taarab ya kale lakini taarab ya kisasa hali hii imekiukwa kwa kiasi fulani. Mfano wa matumizi ya maneno kwa njia hii inabainika katika wa wimbo wa *Kibiriti Upele.* Mwanamume muasherati anaambiwa na mke wake ajipime ili athibitishe kama ana ugonjwa wa ukimwi:

*Kama kweli wanitaka nenda kapimwe ukimwi*
*Na uwache mseto na uwache mseto*

Ingawa matumizi ya mafumbo au maneno yenye maana fiche ni kwa kiwango kidogo kiasi katika taarab ya kisasa, mtindo huu bado unatumika.

## 5.2 Matumizi ya Lugha

Uchunguzi wa lugha katika nyimbo za taarab za Zanzibar umeonyesha mielekeo ya jamii kuhusu mwanamke. Moja kati ya mielekeo hii ni kwamba lugha inayomsawiri mwanamke ni ya kumdunisha. Mjadala unaendelea kusema kuwa usawiri huu unabainika katika matumizi ya maneno na tamathali za usemi. Usawiri wa mwanamke kupitia kwa maneno na tamathali umepata kushughulikiwa na Kramarae na wenzake (1983). Kramarae na wenzake (1983:9) wanakubali kwamba lugha ya tamathali imetumiwa na wanaume kumsawiri mwanamke. Wanaendelea kushikilia kuwa wanaume wanaoendelea kuwahususha wanawake na viungo vya mwili wa binadamu, matunda, wanyama ama kuwa na tabia za kitoto wanadhihirisha mwelekeo wao kwa wanawake. Kwa maoni yao mwelekeo huu husaidia kudumisha hali inayomkweza mwanamume na kumdhibiti manamke. Kwa maoni yetu mawazo haya ya akina Kramarae

yanaonekana yakiwa potovu kwa sababu yanakisia kuwa tamathali zozote zinazotumiwa kumsawiri mwanamke ni za kumdunisha ilhali tujuavyo ni kuwa katika tamaduni nyingi, usawiri wa wanawake kwa njia hii wakati mwingine huwakweza wala sio kinyume.

Katika jamii ya Waswahili mwanamke analinganishwa na baadhi ya mimea kama vile maua na matunda; vilevile na ndege na wanyama. Usawiri huu hauna maana kwamba unamdunisha mwanamke. Njiwa na makinda wa ndege kwa mfano, huchukuliwa kuwa ni ndege wapole na ambao ni waaminifu, koa hupewa sifa za uwerevu, embe ni tunda tamu na ziwa ni sehemu ya mwili iliyo na umuhimu kama chemichemi ya uhai wa mtoto. Vitu hivi vyote vya kimaumbile vikitumiwa kumsawiri mwanamke huonyesha kuwa jamii inamkweza mwanamke.Mtazamo huu wa kuwalinganisha wanawake na viumbe katika jamii ya Waswahili unaripotiwa kutumika katika miaka ya 1960. Mfano unabainika katika wimbo wa *Waridi Lisilo Ua*. Wimbo huu ulitungwa na marehemu Seif Selim, aliyekuwa mwanachama wa klabu ya Ikhwan Safaa Taarab kisiwani Zanzibar mwaka 1960. Lugha aliyotumia mtunzi katika wimbo huu inamwonyesha mwanamke kama kiumbe mrembo na dhaifu, anaendelea kusema kwamba mwanamke katika hali hii anapaswa kulindwa kutokana na ashiki za wanaume wengine nje ya ndoa. Mawazo haya ya Seif (1960) yanaonyesha kwamba jamii ya Waswahili ilianza kupiga hatua kubwa katika mahusiano ya kijamii na kuanza kutetea nafasi ya mwanamke katika nyimbo zake.

Khatib (1992) katika uchunguzi wa nyimbo za taarab za Zanzibar ameonyesha kwamba wanawake walisawiriwa kama maua, ndege na vitu vingine vya kimaumbile. Anaendelea kusema kwamba kuanzia kipindi hicho 1960 vichwa vya nyimbo za taarab nchini Zanzibar vilianza kuwa vya vitu kama vile nanasi, kunguru na ua miongoni mwa mengine.

### 5.2.1 Lugha na Utamaduni

Matumizi ya lugha kulingana na utamaduni ni njia nyingine ya kuonyesha mwelekeo wa jamii kuhusu mwanamke. Utamaduni ni dhana iliyo na fasiri nyingi lakini kwa sababu ya utafiti huu tumetumia fasiri inayoendelezwa na Yule (1996:246) kwamba,

> "Utamaduni ni maarifa anayopata mtu kutoka kwa jamii kwa hivyo kila jamii ina mwonoulimwengu wake"(T.Y).

Utamaduni ni muhimu katika kumfunza mtoto au mtu mzima itikadi za jamii na hutenga nafasi ya kila mmoja. Mitagusano ya wanajamii haiwezi kufanyika pasi na kuwepo kwa lugha na bila ya lugha utamaduni hufa kwa kuwa njia ya kupitisha maarifa, thamani na mambo mengine hukosekana.

Mawazo mengine yanaoeleza umuhimu wa utamaduni katika kukuza lugha ya mtu yanaendelezwa na Halliday (1978:9) kwamba,

> "Kupitia kwa lugha ndipo tunajifunza kuhusu jamii zetu na kushiriki katika shughuli za kijamii kama inavyopasa." (T.Y)

Ni bayana kwamba kila binadamu hutoka katika utamaduni fulani uliyo na dhana na miundo mbalimbali inayotumiwa kuwagawanya watu kwa misingi mbalimbali kama vile ya kijinsia na usawa. Uchunguzi wa kina ukifanywa katika miundo mbalimbali za kijamii itabainika wazi kuwa tamaduni nyingi zimemtengea mwanamke nafasi ya chini akilinganishwa na mwanamume. Mfano unaweza kutolewa kwa neno la kikalenjin '*muren*' linalotafsiriwa mwanamume, jina la mtu mzima wa jinsia ya kuime; jina hili linapotumika kumrejelea mwanamke maana hubadilika. Maana katika msingi huu ni kuwa mwanamke ni kiumbe duni na asiye na ujasiri ilhali mwanamume katika jamii hii anahusiswa na ujasiri. Neno '*muren*' likitumika kumtajia mwanamke basi mwanamke huyu ametenda mambo ya ujasiri na anasifiwa kwa kuitwa kwa jina

hilo. Hili ni dhihirisho kwamba maneno fulani hupata maana nyingine tofauti kutegemea utamaduni wa jamii husika na miktadha mbalimbali.

### 5.3 Tamathali za Usemi katika Wimbo wa Kibiriti Upele.

Wimbo wa *Kibiriti upele* unasimulia hadithi ya wahusika watatu. Ingawa mwimbaji hakutaja majina yao tunakisia kwamba ni wa kiume na kike kutokana na yanayosimuliwa. Wahusika wawili ni wa kike na mmoja ni wa kiume. Mwanamke ambaye ni msimulizi ana shida katika ndoa yake kwa kuwa ana mume ambaye si mwaminifu. Mwanamume huyu ana mwanamke mwingine nje ya ndoa na ambaye baadaye anamwambukiza ugonjwa wa ukimwi.

Katika sehemu hii tumeshughulikia kazi yetu kwa kuzingatia uhakiki wa kimtindo katika viwango vya semantiki na kisintaksia ili kuleta maana mpya au kusisitiza wazo fulani. Matumizi ya tamathali ni ukiushi wa kimaksudi wa matumizi ya lugha ili kumwezesha mwimbaji kutoa masimulizi yake kwa njia iliyo na athari kwa wasikilizaji. Katika wimbo huu tamathali mbalimbali zimetumika katika kuwasilisha ujumbe wa mwimbaji kwa hadhira.

Maelezo mengi yametolewa kuhusu maana ya tamathali za usemi. Mfano wa maelezo ya tamathali ya usemi na ambayo tumetumia katika utafiti wetu ni ya Msokile (1993:39) kwamba,

> "Tamathali za usemi ni maneno, nahau, au semi ambazo hutumiwa na waandishi wa fasihi ili kutia nguvu na msisitizo katika maana, mtindo na pengine sauti katika maandishi."

Kwa minajili ya uchanganuzi wetu tumetumia maelezo ya tamathali kuwa ni mbinu za kusisitiza ujumbe wa mwimbaji. Tamathali pia hutumiwa kuipamba kazi ya sanaa ya fasihi. Ingawa tamathali ni nyingi tumezijadili baadhi tu zilizotumika katika data yetu.

### 5.3.1 Tashbihi

Hii ni tamathali ambayo vitu viwili au zaidi vyenye sifa tofauti hulinganishwa kwa kutumia maneno kama vile kama, mithili ya, sawa na na kadhalika.

Katika mstari wa nne ubeti wa mwisho kuna tashbihi:

> *Hamo tena hesabuni* ***kama jibwa la sokoni***

Mwimbaji amezifananisha tabia za mwanamume na mbwa wa sokoni jinsi anavyozurura. Mwimbaji anachukizwa na tabia ya mwanamume ya kuzurura akiwatafuta wanawake mitaani bila ya kujali yule atakayekidhi ashiki zake. Mwanamume hatimizi wajibu wake nyumbani kwa mkewe lakini aliamua kuwatafuta wanawake wengine nje ya ndoa na mwishowe anabaki amesononeka na upweke baada ya ndoa yake kuvunjika.Mbwa wa sokoni ni yule asiyetakikana kumkaribia mfanyibiashara yeyote.Mwanamume kwa kulinganishwa na mbwa wa sokoni anaonyeshwa kufukuzwa na wanawake kwa kuwa hatakiwi tena.

### 5.3.2 Kinaya/Kejeli

Tamathali hii hutumia maneno ambayo kwa kawaida huwa ni kinyume kabisa na maana inayotolewa na maneno hayo. Maneno ya kukejeli ni ya kutia uchungu na ya kutamausha. Kuna aina mbili za kinaya, kinaya rahisi na kinaya cha maelezo.

Ufafanuzi wa kinaya unaofaa katika mjadala huu ni ule unaoshikiliwa na Fowler (1996:117) kwamba,

> "Kinaya ni mbinu ya kuwasilisha ujumbe kwa hadhira wa aina mbili, hadhira ya kwanza ni ile iliyo na ufahamu na inajua lengo la msemaji. Hadhira ya pili ni ile isiyojua wala kufahamu nia ya msemaji na huchukulia maana ya nje."(T.Y)

Tumetumia aina ya kwanza ya hadhira ambayo inafahamu lengo la mwimbaji. Kejeli iko katika mstari;

kamfate hana choyo wala ye muhali hana.

Mwanamke anamwelekeza mumewe muasherati kwa mwanamke muasherati kwa njia ya kejeli. Anamdanganya kwamba yule mwanamke ni mkarimu na yuko tayari kuwa na mwanamume yeyote. Linalotokea baadaye ni kuwa kumbe mwanamke muasherati alikuwa na virusi vya ukimwi na anamwambukiza yule mwanamume.

### 5.3.3 Misemo

Misemo ni kauli za mafumbo.Hutumia kauli za kawaida zinazositiri maana na hutumika kulingana na utamaduni wa jamii inayohusika.Kwa kuwa misemo ni zao la jamii,jamii huuelewa undani na uzito wa misemo.

Maneno ya misemo yanabainika katika mistari mbalimbali ya wimbo wa Kibiriti Upele. Katika mstari unaofuata,

***Nenda mwingine sikosi wa mbili havai moja***

Msimulizi anatumia msemo**; wa mbili havai moja,** kwa maana kuwa kama mtu amezoea kiwango fulani cha maisha hawezi kubadilisha.Hapa mwanamke anasema kuwa hata kama atamwacha mumewe atampata mume mwingine wa kiwango cha mumewe ambaye atampenda na kumtimizia mahitaji yake.

Kupitia kwa mbinu hii ya misemo tunagundua kwamba mwanamke anaweza kufanya maamuzi kwa mambo mengine kama uhusiano katika ndoa baina ya mwanamke na mwanamume.

### 5.3.4 Sitiari

Matumizi ya sitiari ni njia nyingine muhimu na hutumiwa na jamii kurejelea mwanamke pia wanaume. Hii ni mbinu ambayo vitu viwili vilivyo tofauti kitabia na kimaumbile huhusishwa kwa njia moja. Kitu kimoja husemwa ni kingine. Hii ina maana kwamba msingi wa sitiari ni uhamisho wa maana.Wamitila (2008) anasema,

> "Sitiari huwa na maana fiche".

Katika wimbo huu, sitiari kadhaa zimetumiwa kuwalinganisha baadhi ya wahusika wa kiume na wa kike. Mwimbaji amemlinganisha mwanamke na viumbe au vitu mbalimbali. Katika baadhi ya mistari mwimbaji amewapa nafasi wahusika wawalinganishe wahusika wenzao na viumbe wengine. Mwanamke aliyetengana na mumewe anamlinganishe yule aliyempokonya mume na kibiriti upele. Upele ni ugonjwa wa uvimbe na kibiriti ni dawa. Sitiari husaidia kukisia uwezo wa wahusika hao.

Mwanamke anayelinganishwa na kibiriti upele ni mnyonge na anajaribu kujiegemeza kwa mume wa mtu ili afaidi kiuchumi. Mwanamke huyu pia ni dawa ya mwanamume mwenye kutangatanga. Mwanamke wa pili, ambaye ameolewa anaonekana kuwa na uwezo wa kuamua kumwacha mume muasherati. Mwanamke huyu wa pili, ni kiwakilishi cha mwanamke wa kisasa ambaye anapigania nafasi yake na anafaulu. Katika utafiti huu tumechukulia kuwa sitiari hizi zimetumika kuinua hadhi ya mwanamke licha ya kuwa kuna baadhi zinazodunisha wahusika wa kike. Kama ilivyobainika katika data iliyokusanywa, wanawake wanalinganishwa na vitu vingine kwa njia ya sitiari. Tumejadili matumizi ya sitiari za bidhaa, chakula, ndege na mimea katika wimbo wa Kibiriti Upele.

#### 5.3.4.1 Bidhaa

Kichwa cha wimbo, *Kibiriti Upele* ni sitiari. Ndani yake kuna sitiari ya kibiriti upele. Katika kamusi ya Kiswahili sanifu (1981:156) kibiriti ni "aina mojawapo ya dawa ya upele" na "upele ni vituruturu vilivyozagaa katika mwili aghalabu huwasha na kutunga usaha." Mwanamke kama kibiriti upele yuko mbioni kuwatafuta wanaume ili apate kuwakidhia haja zao. Mahitaji haya ya mwanamke katika wimbo huu ni ya aina mbili, kwanza ni ashiki za kimwili na pili, ni mahitaji ya fedha. Mahitaji haya yanamzuia mwanamke huyu kutulia lakini hafichi azma yake ila yuko mbioni katika kujaribu kuyakidhi. Sitiari hii inaonyesha kuwa mwanamke muasherati hatosheki kamwe na hali yake ila atatumia kila mbinu ili mahitaji yake yapate kutimizwa.

Sitiari nyingine inapatikana katika mstari,

***Maarufu kifyagio yeye jamvi la vijana***

Kifyagio ni sitiari ya uchafu wa mwanamke anayejihusisha na uasherati. Jamvi ni mkeka wa kitamaduni unaoshonwa ili ukaliwe. Ufagio kulingana na kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981:424) ni kifaa kilichotengenezwa kwa njuti, unyasi au makumbi kinachotumiwa kuondolea taka sakafuni au ardhini. Mwanamke anayelinganishwa na ufagio ni asherati kwa kushiriki ngono na wanaume mbalimbali ni kama jamvi la vijana, anashiriki tabia hii ya ngono na vijana wa umri mdogo ukilinganishwa na umri wake.

Sitiari hizi zimetumiwa na mwimbaji ili kumsuta mwanamke huyu kwa nia ya kumuonyesha kuwa tabia yake chafu inawachukiza wanajamii na inafaa abadilishe.

#### 5.3.4.2 Chakula

Misamiati mingi ya kumtajia mwanamke inapatikana katika jamii. Hii inatokana na imani kwamba mwanamke ni kiumbe dhaifu ambaye anahitaji kubembelezwa kinyume na wanaume. Mistari ifuatayo ina baadhi ya sitiari zinazomlinganisha mwanamke na vyakula;

> ***Wako wa nusu chipsi*** *zege lenye hali moja*

Mwanamke amelinganishwa na nusu chipsi. Chipsi ni aina ya chakula kinachopendwa sana. Ni viazi vilivyokatwakatwa na kukaangwa kwa mafuta.

Kulingana na wataalam wa lishe, chakula hiki husemekana kuwa hakina viungo vyote muhimu vya lishe. Ujinga wa mwanamke unabainika kuwa ni rahisi kumpata kwa kununuliwa vitu vidogo kama chipsi. Ingawa mwimbaji amemchora mwanamke huyu kama muasherati anamtumia kumkashifu mwanamume kwa kuyathamini mambo madogo ambayo hayana thamani ya kudumu kama zilivyo chipsi.

### 5.3.5 Takriri

Takriri ni mbinu ya kurudiarudia silabi, neno, mistari na vifungu. Nia ya mtunzi ya kutumia mbinu hii ya takriri ni kusisitiza jambo fulani. Mbinu hii ni muhimu sana katika nyimbo za Kiafrika. Mawazo haya ya takriri yamezungumziwa na Finnegan (1970:163). Katika uchunguzi wake wa ushairi wa Kiafrika aligundua kuwa kuna takriri nyingi sana. Anaendelea kusema kwamba licha ya mbinu hii kuwa na athari za kiujumi, ina manufaa ya kimtindo katika wimbo.

Matumizi ya mbinu ya takriri inabainika katika ubeti:

> *Changanya changanya changanya changanya,*
> *Kibiriti upele hunichanganyi naye,*
> *funganya funganya funganya funganya*

*Kibiriti upele hunifunganyi naye*
*Shindana shindana shindana shindana,*
*Kibiriti upele sishindani naye,*

Mwanamke katika mistari hii minne anasisitiza kuwa hawezi kukubali mumewe awe na wanawake wengine nje ya ndoa.Na kama tulivyosema hapa juu kwamba kibiriti upele ni usawiri wa mwanamke muasherati, msimulizi hataki uhusiano wowote naye. Kwa kufanya hivi, mwanamke anatetea nafasi yake katika jamii.

Takriri zingine ni kama vile;kibiriti upele,hujipendi najipenda hujitaki najitaka,basi,mchukue mchukue mchukue na zingine.Takriri hizi hutumiwa kwa lengo la kusisitiza ujumbe wa mwimbaji.Mwanamke anakataa katakata kujihusisha na tabia ya mumewe ya uasherati.

**5.3.6 Maswali ya Balagha**

Maswali haya huulizwa na mwimbaji ili kusisitiza ujumbe unaowasilishwa kwa wasikilizaji. Maswali haya huchochea hadhira ili iweze kutafakari kuhusu maudhui yanayowasilishwa. Linalofuata ni swali la balagha lililotumiwa katika wimbo huu.

Swali lake yeye huyo una hela huna?

Swali hili lasemekana na mwimbaji kuwa linaulizwa na mwanamke asherati. Mwanamke huyu anamwuliza mwanamume yeyote aliye na haja naye kama ana fedha za kumpa. La msingi hapa ni kuwa mwanamke asherati hampendi mwanamume asiye na mali kwa kuwa ni mnyonge. Licha ya kujua kuwa kuna wanaume wazuri wasiokuwa na mali, haja yake haikuwa ni kumpata mwanamume mzuri bali haja yake ni kupata mali ya kumfaidi.

### 5.4 Tamathali katika wimbo wa *Tupendane Wabaya Waulizane*

Wimbo huu umeimbwa na Mzee Yusuf. Wimbo wa *Tupendane* ni wimbo wa mapenzi. Mwimbaji ambaye tumemchukulia kuwa ni msimulizi anamshauri mpenzi wake wa kike kuhusu maswala mbalimbali. Maswala haya ni pamoja na jinsi ya kumhudumia mumewe katika ndoa na kukataa kusikia maneno ya watu ili penzi lao lipate kuimarika na kudumu. Mwimbaji anaijulisha hadhira kuwa kuna mahasidi wasiofurahia watu wawili wakipendana katika ndoa na anawaonya wenye tabia kama hii katika jamii kuwa wataumiza mioyo yao bure.

Wimbo huu kama ulivyo wimbo wa *Kibiriti Upele* umetumia tamathali za usemi mbalimbali.

#### 5.4.1 Tashbihi

Mbinu hii inabainika katika mstari,

> *Wale wenye roho mbovu* ***watakonda kama uzi***

Msimulizi ametumia mbinu hii ili kuwakejeli baadhi ya wanajamii wanaotumia hila ili kuwatenganisha wanaopendana. Anaendelea kuwashauri wanaopendana waendelee kudhibiti uhusiano wao na wakifanya hivyo mahasidi hawana lingine ila kubaki kuwa na hisia za kero zitakazowakondesha sana. Jamii inaonywa dhidi ya kuwatenganisha wapendanao bali iendelee na kuwaunganisha.

#### 5.4.2 Sitiari

Sitiari nyingi zimetumika katika wimbo huu kama ilivyo wimbo wa kibiriti upele.Sitiari hizi zimegawanywa katika makundi mbalimbali.

#### 5.4.2.1 Cheo

Watu wanaweza kulinganishwa na wenye vyeo katika shughuli za kijamii kama vile kazi. Cheo kulingana na kamusi ni daraja ya mtu katika kazi. Kazi zinazoenziwa hutumiwa katika kuzilinganisha na tabia za watu wanaoheshimiwa. Katika wimbo huu sitiari hii inabainika katika ubeti :

*Oh Habiti wangu usipunguze dozi mimi bado sijapoa*
*Daktari wangu dawa zako wewe ndo zitonisaidia,*
*Ah sweetie asubuhi nikiwa hoi wayaja na makamusi*

Mwanamke analinganishwa na daktari. **Daktari** huwatibu wagonjwa kwa dawa na kuwaelekeza jinsi ya kuzitumia dawa hizo. Maana ya sitiari daktari ni kwamba mwanamke ana uwezo wa kukidhi mahitaji yote ya mwanamume na ni tegemeo lake.Katika mfano huu, mwanamume anaonyeshwa kama kiumbe dhaifu na anayemtegemea mwanamke.Mwanamke kwa upande mwingine amepewa nafasi yake.Bila ya mwanamke, mwanamume hawezi kujitegemea.

#### 5.4.2.2 Bidhaa

Bidhaa nazo zinatumika kumchora mwanamke.Bidhaa inayobainika ni kamusi. Maana ya kamusi ni kitabu cha maneno yaliyopangwa kwa utaratibu wa alfabeti na kutolewa maana na maelezo mengine. **Kamusi** katika msingi wa kiusomi ni chemichemi ya maarifa. Kumlinganisha mwanawake na kamusi ni kuonyesha kwamba ana maarifa ya maneno yanayoweza kuyeyusha hisia za mwanamume na kumfanya amheshimu na hata kujitengea nafasi yake.Sitiari hii inapatikana katika mstari;

*sweetie asubuhi nikiwa hoi waja na makamusi*

Uwezo huu wa kimaumbile utamwezesha mwanamke kujitengea nafasi yake kama anavyosema Amadiume (2002:44) kuwa,

> "Wanawake katika utamaduni wa jamii ya Wannobi walijitengea nafasi yao na kuwafanya washiriki katika mambo ya utamaduni".

### 5.4.2.3 Chakula

Chakula ni kitu muhimu katika kudumisha uhai wa binadamu.

Aina ya vyakula vinavyorejelewa ni vile vilivyo na utamu na vya kusisimua. Mistari mbalimbali ina mifano ya sitiari hizi :

*Sweetie usiku unibembeleze uje mwema usingizi,*
*Honey taratibu unilaze tukutane kwenye njozi,*
*Honey basi unipe chai yenye nyingi tangawizi,*

**Peremende** *(sweet),* na **asali** *(honey)* ni vyakula vilivyolinganishwa na mwanamke.Uzuri wa mwanamke unadhihirishwa na maneno peremende na asali. Mwanamke huyu humfurahisha mpenziwe wa kiume kwa upishi, maneno matamu na mapenzi. Kupitia kwa njia hizi mwanamke amejitengea na kutetea nafasi yake.

### 5.4.2.4 Mimea

Wanawake wanalinganishwa na mimea au sehemu kama maua na matunda. Mimea na maua huongeza nakshi katika mazingira na huhitaji kutunzwa kwa uangalifu. Vivyo hivyo mwanamke ni wa manufaa katika jamii lakini anahitaji kuungwa mkono na jamii ili aweze kujisimamia, kama anavyosema Eagleton (1991:7) akirejelea maoni ya Woolf, Moi na Showalter kwamba, kinachomfanya mwanamke kuonekana tofauti ni kukosa kuungwa mkono kijinsia na kijamii, ukosefu wa elimu ya kutosha, ukosefu wa mali, na uoga. Katika wimbo huu mwanamke

ameungwa mkono na mwanamume katika kutetea nafasi yake kwa kuelimishwa jinsi ya kumdhibiti mwanamume. Mmea unaotajwa ni tunda katika mstari:

*Tunakula tunda bivu kwa manakshi na mapozi*

Tunda bivu ni sitiari ya mapenzi au tendo la ngono ambalo hutumiwa kumfurahisha mwanamume.

#### 5.4.2.5 Ndege

Mwanamke anafananishwa na ndege na anapendwa sana na mumewe. Mwimbaji anamshauri mwanamke huyu kuwapuuza wanajamii walio na nia ya kuwatenganisha.Sitiari hii inapatikana katika mstari;

*Ah Ayuni wangu wapuuze hao*

#### 5.4.2.6 Michezo

Mahusiano katika jamii yanaweza kulinganishwa na shughuli za kila siku kama vile michezo.Mwimbaji anamwambia mpenzi wake kuwa wawaonyeshe walionuia kuwatenganisha kuwa kamwe hawatawachana.Sitiari hii inatokea katika mstari;

*Wazushi tuwaringie* ***timu yetu kali kwa mechi.***

### 5.4.3 Maswali ya Balagha

Mbinu hii inabainika katika sehemu ya mwisho. Mwimbaji anawaonya baadhi ya wanajamii wasiowafurahia wanaopendana kwamba,

*Kama shubiri ni tamu asali ina ladha gani?*

Asali ni sitiari ya furaha na ufanisi wa maisha na shubiri ni ya msukosuko.Licha ya maisha kuwa na uchungu wa shubiri ni lazima yavumiliwe.Mwimbaji anasema kuwa hata wakipata shida

maishani bado maisha ni mazuri.Na je kukiwa hakuna matatizo maisha yatakuwaje? Baadhi ya wanajamii wenye tabia ya kutengana maisha yakiwa magumu wanasutwa kupitia kwa sitiari kama hii.

### 5.4.4 Misemo

Misemo ni kauli za mafumbo. Misemo hutumia kauli za kawaida zinazositiri maana na huambatana na utamaduni unaohusika. Kila utamaduni una misemo yake inayoafikiana na itikadi, mila na desturi. Kwa kuwa misemo huandamana na jamii, jamii husika huuelewa undani na uzito wa misemo kama inavyostahiki.

Misemo imetumika katika mistari:

*Huyu kanitia wazimu vinenoneno punguzeni.*

Msemo **kanitia wazimu** inaonyesha kuwa msimulizi ameathirika kihisia. Anampenda mpenzi wake kiasi cha kukosa kujizuia. Kwa kuwa mwimbaji ni mwanamume hatuna budi ila kusema kuwa amedhibitiwa na mkewe. Mwanamke amepata nafasi yake.

Misemo zaidi ni kama vile, wabaya wetu **macho wameyakodoa**, **liwaume penzi hili**, tuwaone wenye wivu **wanapojitia vitanzi** na kadhalika.Kukodoa macho imetumika kuonyesha hali ya watu ya kuchunguza mambo yasiyowahusu kwa nia ya kuwasababishia maafa.Msemo **liwaume penzi hili** ina maana kuwa kuna watu ambao hawahisi vizuri wanapowaona wenzao wakiishi kwa amani.Watu wa aina hii husumbuka mioyoni mwao.**Kujitia vitanzi** ni hali ya kujitoa uhai.Hali kama hii husababishwa na hisia za kuwaonea wengine wivu na kujisababishia machungu kutokana na ufanisi wao.Mwimbaji anawasuta watu kama hawa kwa kuwaambia kwamba wanaweza kufa kwa sababu ya kuona wivu.Msemo mwingine katika mstari;

*Wale walotupangia na kutuletea majungu*

ni **kutuletea majungu.** Msemo huu unarejelea wale watu ambao ni mahasidi na wanaojaribu kuwatenganisha wanaopendana kupitia kwa njama wanazowapangia. Mwimbaji anawaonya kuwa watapata adhabu kutoka kwa Maulana.

Misemo imetumiwa kuionya jamii dhidi ya kuingilia kati na kusababisha mizozano baina ya watu wawili wanaopendana.

### 5.4.5 Takriri

Hii ni mbinu ya kurudiarudia maneno, sentensi na silabi. Takriri hutumiwa na mwimbaji ili kusisitiza ujumbe na kumfanya msikilizaji aathirike. Katika wimbo huu kuna ukariri wa kifungu,neno na silabi. Kifungu cha kiitikio kinakaririwa kuonyesha umuhimu wa kuwa na ushirikiano na mapenzi ya watu wawili. Utawakinga dhidi ya mahasidi:

> *Wawili wakipendana adui hana nafasi*
> *Mbona mtaumwa sana nyie wabaya wa nafsi*.

Takriri ya silabi pia imetumika, kama katika kufungu

> *waulizane, wanong'one, wasilione na wasizione.*

Silabi hizi zinatokea mwisho wa mistari au katika maneno kwenye kifungu kimoja. Silabi **ne** na **wa** zimerudiwarudiwa ili kudhihirisha sifa za ushairi katika wimbo.

## 5.5 Hitimisho

Tumechunguza matumizi ya lugha ya tamathali katika nyimbo mbili za taarab ili kuonyesha jinsi maudhui ya nafasi ya mwanamke yanavyoshughulikiwa na waimbaji kupitia kwa lugha hii. Zaidi ya hayo tumeweza kuonyesha jinsi lugha inavyoweza kutumiwa kuonyesha mwelekeo wa jamii kuhusu jinsia ya kike na kiume.

Kwa kuwa swala la jinsia ni zao la jamii, mielekeo ya jamii kuhusu jinsia ya kike hupitishwa kwa wanajamii kupitia kwa lugha. Lugha iliyotumiwa kumrejelea mwanamke katika nyimbo zote inaonyesha mwelekeo chanya. Mwanamke amechorwa kama mwerevu na mshikilizi wa asasi ya ndoa kutokana na kuwa adilifu na mwenye bidii.Ameweza kukidhi mahitaji ya jamii. Kwa kufanya hivi anatetea nafasi yake. Katika wimbo wa *Kibiriti Upele*, mwanamke anamwonya mwanamume dhidi ya utamaduni unaomruhusu kuwa na wake wengi, anaitisha talaka na hata kujisimamia bila ya msaada wa mumewe.

Katika wimbo wa *Tupendane Wabaya Waulizane*, mwanamke anasawiriwa kama kiumbe anayetetewa na jamii. Anahimizwa amtunze mumewe kwa mapishi, maneno matamu na mambo mengine. Anaendelea kushauriwa asiyasikilize maneno ya mahasidi wenye nia ya kumtenganisha na mpenziwe.

Kutokana na yaliyobanishwa, ni bayana kuwa nyimbo husaidia katika kuendeleza juhudi za kumtetea mwanamke dhidi ya ukandamizaji kama tulivyoona katika sura hii.

# SURA YA SITA:

# MUHTASARI WA MATOKEO

## 6.0 Utangulizi

Nia yetu katika sura hii ni kutoa muhtasari wa matokeo ya utafiti wetu. Kutokana na matokeo ya utafiti wetu tumeweza kujadili nadharia tete zetu pamoja na kuangazia matatizo ya utafiti wetu.Mwisho, tumetoa mapendekezo ya tafiti za baadaye.

## 6.1 Muhtasari wa Matokeo

Lengo kuu la utafiti wetu lilihusu uchanganuzi wa nafasi ya mwanamke katika nyimbo mbili za taarab za Zanzibar. Nyimbo hizi mbili za *Kibiriti Upele* na *Tupendane Wabaya Waulizane*, ziliimbwa na Mwanaidi Shaaban na Mzee Yusuf. Nyimbo hizi zinaangazia maswala ya kijamii yanayomzingira mwanamke. Ingawa nyimbo za taarab zimeshughulikiwa na wahakiki wengi swala la kutetewa kwa nafasi ya mwanamke halijahakikiwa kwa kina.

Sura ya kwanza ya utafiti ilishughulikia utangulizi, madhumuni na nadharia tete. Aidha yaliyoandikwa kuhusu mada yalijadiliwa na msingi wa nadharia ilishughulikiwa,halafu baadaye njia za ukusanyaji wa data zilibainishwa.Sura hii ilikuwa ndio msingi wa kazi yetu.

Katika sura ya pili, tulitoa maelezo mbalimbali kuhusu aina mbalimbali za nyimbo kiuamilifu. Mifano michache ya vifungu kutoka kwa data ya utafiti ilitolewa ili kuyapa msingi maelezo ya nyimbo. Baadhi ya nyimbo hizi ni za unyago, harusi, maadili na zingine. Nyimbo kama fani ya fasihi simulizi hutumiwa kuwasilisha ujumbe katika tamaduni nyingi za Kiafrika; vivyo hivyo nyimbo za taarab huwapa fursa wanawake kupitisha sauti zao kwa jamii.

Sura ya tatu na nne zilichanganua maudhui ya nafasi ya mwanamke katika nyimbo za taarab. Katika sura ya tatu uchanganuzi wa maudhui ulijikita katika wimbo wa *Kibiriti Upele* na *Tupendane Wabaya Waulizane* ulifanywa katika sura ya nne.

Katika sura ya tano tulijikita katika lugha. Tumejadili jinsi tamathali tofauti tofauti zimetumika katika nyimbo za taarab kuendeleza maudhui ya nafasi ya mwanamke. Tumeonyesha matumizi ya tamathali hizi katika beti na mistari mbalimbali ya nyimbo hizi na maana ya kila tamathali ilitolewa kulingana na muktadha wa matumizi. Tumegundua kuwa waimbaji wametumia tamathali hizi ili kuwasilisha ujumbe kwa njia inayoathiri hadhira.

Utafiti huu umejikita katika nyimbo mbili zilizokusanywa kutoka kwa taarab ya Zanzibar ingawa nyimbo zingine zilitajwa hapa na pale. Hizo zilizotajwa zinapatikana katika sehemu ya kiambatisho.

### 6.1.1 Upimaji wa Madhumuni

Utafiti huu umefanywa kwa madhumuni ya kuonyesha:

- Jinsi waimbaji wa nyimbo mbili teule za taarab wanavyotumia lugha ya tamathali katika kuendeleza maudhui ya uteteaji wa nafasi ya mwanamke katika jamii.
- Kwamba mwanamke amefaulu katika kutetea nafasi yake kupitia kwa nyimbo hizi.
- Kuwa jamii ikiwemo wanaume na wanawake imechukua jukumu la kuitetea nafasi ya mwanamke.
- Ufaafu wa nadharia ya ufeministi wa Kiafrika katika kuzichunguza nyimbo mbili teule za taarab.

Madhumuni haya yote yamebainishwa katika utafiti na kuonyesha kwamba waimbaji wote, wa kiume na kike wametetea nafasi ya mwanamke katika nyimbo zao. Tuligundua kuwa waimbaji wametumia tamathali kadhaa katika kufanikisha maudhui. Kutumika kwa tamathali na waimbaji ni kwa madhumuni ya kuwasilisha ujumbe. Ufaafu wa nadharia ya ufeministi wa Kiafrika ulipimwa na kuonekana kuwa unafaa katika kuzihakiki nyimbo hizi za taarab.

Tumeweza kuthibitisha kwamba utamaduni ndicho kizingiti kikuu katika harakati za kujitetea kwa mwanamke kwa kumtengea nafasi ya chini katika jamii. Juhudi madhubuti lazima zifanywe ili kuchuja zile tamaduni zinazofaa kwa mwanamke na kuziendeleza ili ufanisi uweze kufikiwa.

## 6.2 Upimaji wa Nadharia Tete

Tuliloshughulikia katika utafiti huu ni uchambuzi wa maudhui ya nafasi ya mwanamke katika nyimbo za taarab. Nadharia tete zetu zilikuwa nne. Nadharia tete ya kwanza ilihusu mbinu za uteteaji wa nafasi ya mwanamke. Hili limebainika kuwa ni kweli katika nyimbo za *Kibiriti Upele* na *Tupendane Wabaya Waulizane*. Mbinu hizi ni kama vile kupinga utamaduni unaomruhusu mwanamume kuwa na wake wengi na hata kuitisha talaka kwa mwanamke. Mwanamke aliyeyafanya haya anaepuka kuambukizwa ugonjwa wa ukimwi na mumewe aliyekuwa muasherati. Katika wimbo wa pili, mwanamke anamdhibiti mumewe kupitia kwa chakula na maneno matamu na kumfanya ajitengee nafasi yake.

Pia ilichukulia kwamba uteteaji wa nafasi ya mwanamke unadhihirika katika lugha ya waimbaji. Tamathali zilizotumiwa na waimbaji ni kama vile sitiari,semi,kejeli,tashbihi na takriri miongoni mwa tamathali zingine.Hili limethibika kuwa lina mashiko kwa sababu lugha hutumika kuwasilisha maudhui kwa hadhira.

Nadharia tete ya pili ni kuwa mwanamke anaweza kutetea nafasi yake yeye mwenyewe. Hili pia linadhihirika kuwa kweli katika wimbo wa *Kibiriti Upele*. Mwanamke anaamua kumwitisha mwanamume talaka bila ya kuhimizwa wala kulazimishwa na yeyote. Alijionea mwenyewe hatari iliyokuwa imemkodolea macho na kuamua kujinusuru.

Katika wimbo wa *Tupendane Wabaya Waulizane*,mwanamke hajajitokeza wazi katika kupigania nafasi yake licha ya kupatiwa mbinu mbalimbali na mwimbaji.Mifano ya mbinu hizo ni kama vile upishi wa vyakula na matumizi ya lugha tamu na ya unyenyekevu.Matokeo ya juhudi hizi hazijabainika.

Tatu, ilibainika kuwa jamii ina jukumu kubwa la kutetea nafasi ya mwanamke ingawa bado kuna pingamizi tele. Mwanamke kwa upande wake hajajitokeza wazi kupinga hali hii ya kunyimwa nafasi,huku baadhi ya wanajamii wanaendelea kupinga juhudi za wale wanaotetea nafasi ya wanawake.Haya yanadhihirishwa na mwimbaji wa nyimbo ya *Tupendane Wabaya Waulizane*.Matokeo haya yanafanya nadharia tete inayosema jamii imelegeza juhudi za kutetea nafasi ya mwanamke kuwa ni kweli. Katika wimbo, *Tupendane Wabaya Waulizane*, mwanamke bado anatumika kama kijakazi nyumbani na pia wa kukidhi ashiki za kiume. Ingawa mwimbaji ambaye ni wa jinsia ya kiume anamhimiza mwanamke kutumia mbinu zilizotajwa hapa juu ili kutetea nafasi yake, kuna pingamizi kutoka kwa jamii. Mwanamke anaonywa dhidi ya kuwasikiliza baadhi ya wanajamii ambao wana njama ya kuwatenganisha wanaopendana.

Mwisho, ufaafu wa nadharia ya ufeministi wa Kiafrika katika kuzihakiki nyimbo za taarab ni wa kweli kwani mambo mengi yanayoshughulikiwa na yanayowaathiri wanawake yanatokea katika jamii ya Kiafrika. Maswala haya ni pamoja malezi, mapenzi na ndoa.

Ingawa nyimbo za taarab zimepiga hatua katika kutetea nafasi ya mwanamke changamoto tele bado zinazuia kufikiwa kwa ufanisi. Data imebainisha kwamba mwanamke bado anasawiriwa kwa njia hasi, mfano katika *Kibiriti Upele* ni kuwa mwanamke mmoja amechorwa kama muasherati na mtegemea mwanamume na yuko radhi kufanya lolote ili ampate; hana maadili. Katika wimbo wa *Tupendane Wabaya Waulizane*, jukumu la mwanamke ni kumfurahisha mumewe kwa chakula na ngono na wala hatujaonyeshwa matokeo ya juhudi hizi.
Je mwanamke ametetewa katika nyimbo hizi? Jawabu hapa ni la na ndio. Ndio katika wimbo wa kwanza na la katika wimbo wa pili.

## 6.3 Changamoto za Utafiti

Kwa kuwa sampuli tuliotumia ni sampuli lengwa, kazi yetu ilikumbwa na changamoto mbalimbali.Kwanza kanda za video na tepurekoda tulizozikusanya zilikuwa nyingi na za kukanganya.Ilitulazimu kuchukuwa muda mrefu kuzisikiliza na kuzichuja zile zilizofaa kwa kazi yetu.Pili,ukosefu wa fedha za kuwezesha usafiri hadi sehemu ambayo ni chimbuko la data lilikuwa tatizo lingine; pia gharama ya kununua kanda hizi ni ghali. Mwisho muda wa utafiti ulikuwa mfupi kuweza kupata habari zote zilizotakikana.

Changamoto ambazo tumezitaja ni baadhi tu ya changamoto tulizokumbana nazo katika utafiti. Licha ya changamoto hizo tuliweza kukusanya data zilizotufaa.

## 6.4 Mapendekezo

Utafiti huu ulihusu maudhui ya kutetewa kwa nafasi ya mwanamke katika nyimbo mbili za taarab.Tumegundua kuwa kwa kiasi, bado mwanamke amedunishwa kwa kutengewa nafasi ya chini kama kumpikia mumewe, kumtii na kumfurahisha ili ndoa ipate kudumishwa. Licha ya ufahamu huu, tunapendekeza kuwa tafiti zingine zifanywe kuhusu usawiri wa wanawake katika nyimbo za taarab. Aidha utafiti ufanywe kuhusu chimbuko la taarab ya kisasa na ufanisi wake kama fani ya fasihi simulizi kwa misingi ya nadharia mbalimbali.

Kwa sababu tumetumia nadharia ya ufeministi wa Kiafrika katika kazi nzima na kipengele cha tamathali za usemi katika uhakiki wa kimtindo katika sura ya tano, kazi hii pia huweza kushughulikiwa na watafiti wengine kwa kutumia nadharia nyingine tofauti.

## MAREJELEO


Abdulaziz, M. H. (1979) *Muyaka: 19th Century Swahili Popular Verse* Nairobi, Kenya Literature Bureau

Abedi, K. A. (1969) *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* Dar-es-Salaam, .A. Publishing House

Adeola, James (1990) *In Their Own Voices: African Women Writers Talk* London: James Currey Limited.

Akivaga, S. K. and Odega, B. (1982) *Oral Literature: A School Certificate Course* Nairobi: Heinmann.

Allen, J. (1976) "*Swahili History Revisited*". Unpublished Seminar Paper. Institute of African Studies, University of Nairobi.

______________ (1976) "*Swahilization: A Cultural Concept and Its significance in Kenya Today*". Unpublished Seminar Paper. Institute of African Studies, University of Nairobi

Amadiume,I. (2002) *Bodie, Choices Globalizing Neocolonial Enchantments: African Matriachs and Mammy Water*." Meridins, vol 2: Indiana University Press

Askew, K. (1992) *Performing The Nation: Swahili Musical Performance and the Production of Tanzania National Culture.* Ph.D Thesis, Harvard University

Beauvoir S. (1949*) The Second Sex.* London: Pan Books Publishers.

Beja, S. K. (2001) *Giriama Funeral Songs: A Functional Aesthetic Study* Ph.D Thesis, University of Nairobi.

Besley, (1985) *The Feminist Reader: Essays in Gender and Politics of Literary Cricitism* 2nd Edition. London: Macmillan.

Chesaina, C. (1991) *Oral Literature of the Kalenjin* Nairobi, Heinemann

Con Davis R. and Finke L. (1989) *Literary Criticism and Theory: The Greeks to the Present*. London: Longman Publishers.

Crawford, M. (1995) *Talking Different on Gender and Language.* London, Macmillan

Eagleton M. (1991) *Feminine Literary Criticism*. London: Longman group limited.

Fair,L. (2001) *Pastimes and Politics Culture, Community,and Identity in Post-Abolition Urban Zanzibar*, *1890-1945*: Ohio University Press.

Fowler, R (1986) *Linguistic Criticism.* Oxford: Oxford Universiti Press.

Finnegan, R. (1970) *Oral Litereture in Africa.*Nairobi: Oxford University Press.

Greer, G. (1970) *The Female Eunuch*. New York: McGraw

Hallyday, M. A. K. (1998) *Language as a Socio-Semitic; The Social Interpretation of Language and Meaning* London, Edward Arnold and Stroughton

Harris, L. (1962) *Swahili Poetry* Oxford, Oxford University Press

Imbo, O. (2002 *Oral Traditions as Philosophy*). UK:Rowman and Littlefield Publishers

Indagasi, H. (1988) S*tylistics.* Nairobi: Nairobi University Press

Khatib, M. S. (1987) *"Taarab katika Fasihi Simulizi" katika Makala za Semina ya Fasihi, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.* University of Dar-es-Salaam pg 16-25

____________ (1992) *Taarab Zanzibar* Dar-es-Salaam, Tanzania Publishing House.

Kingei, K. (1993) *Language Culture and Communication: The Role of Taraab Songs in Kenya* 1963-1990 Ph.D Thesis, Harvard University.

_______________(1994) *"Swahili Taarab as a medium of Political Expression in Kenya" in Writers Forum. A Journal of Fine Writers Association of Kenya* Vol. 2; pgs 74-91

Kisiroche, R. (2011) *Sauti ya Mwanamke Dhidi ya Ubabedume Katika Tamthilia Tatu za Kiswahili.* University of Nairobi – haijachapishwa

Knappert, J. (1972) *A Choice of Flowers.* London: Heinmann

Kramarae 1983, Language, Gender and Society/ edied by Barrie Thorne, Cheris Kramarae, Nancy Henley, Cambridge: New Bury House.

Kuhenga,C. (1977) Tamathali za Usemi.Dar es Salaam:East Africa Literature Bureau.

Leech,G.N. (1969) *A Liguistic guide to English Poetry*.Harlow:Longman

Mazrui, A. and Shariff, I. N. (1994) *The Swahili: Idiom and Identity of an African People.* Trenton: N. J. Africa World Press

Millet (1969) *Sexual Politics*. Lindon:Virago

Moi ,T. (1985) *Sexual/Textual Politics; Feminist Literary Theory.* London: Routledge.

Msokile (1993) *Misingi ya Uhakiki ya Fasihi*, Nairobi E.A.E.P

Njogu K. and Chimera R. (1990) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Peter B. (1995) *Beginning Theory: An Introduction to Literary and Cultural Theory* .London: Manchester University Press.

Roberts, S.(1967) *Wasifu wa Siti Binti Saad:*London: Nelson

Steady (1981) Reflecting on the Politics of Sisterhood. New York: African Wordpress

Timammy (2002) *Mombasa Swahili Women's Wedding Songs*: *A Stylistic Analysis*, University of Nairobi. Haijachapishwa.

Topp, J. F. (1992) *Women and Africanization of Taarab in Zanzibar*. Ph.D Dissertation, London, London School of Oriental and African Studies

Trudgill, P. (1995) *Sociolinguistics: An Introduction to Language and Society (3^Rd^ Edition)* London,:Penguin Books

The Daily Nation, (April 2013 DN2: 4)

Tuki (1981) Kamusi ya Kiswahili, Nairobi, Oxford University Press.

Tuki (2000) *English-Swahili Dictionary*. Second Edition. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007); *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila,K.W. (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

______________ (2003) (b) *Kichecheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publishers

______________(2008) Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi. Nairobi: Vide-Muwa Publishers

Veronica (2005), Nafasi ya Mwanamke katika tenzi mbili ya Shabban Robet: Utenzi Hati na Utenzi wa Hati na Utenzi wa Adili Mama. Nairobi University-Haijachapishwa.

Werney, H. (1942) *Taboo: A Sociological Study.* Stanford: Stanford University Press

Whitney, H. W. (1969) *Swahili: The Rise of National Language.* London: Methuel

Wollstonecraft,M.(1792) *A Vindication of the Rights of Women*. UK: Forgotten Books.

Woolf V. 1929- Avindication, A Room of One's own, London: Hogarth

www.standard.co.ke (30/4/2013)

Yule, G. (1996) *Pragmatics.* UK: Oxford University Press

**KIAMBATISHO**

Wimbo 1. **Kibiriti Upele – Mwanaidi Shaaban**

Kama sababu ni huyo akuzuzuaye huyo

Kibiriti upele huyo isikupe taabu basi isikupe

Nenda naye huyo basi nenda naye

Sina haja nawe basi sina haja

Usipate taabu basi, kwenye loji uwe mteja

Usinitilie nuksi mimi nawe sina haja

Wako we wa nusu chipsi zege lenye haLi moja,

Kwangu mi huna nafasi mimi ex aningoja,

Nenda mwingine sikosi x3 wa mbili havai moja

Nina wivu najipenda, naipenda roho yangu

Sihatarishi maisha, siwi nenda rudi kisha

Kama kweli wanitaka x3 nenda kapimwe ukimwi

Na uache mseto na uache mseto.

Hujipendi najipenda hujitaki najitaka

Pendo la shirika mi naliogopa

Changanya changanya changanya changanya

Kibiriti Upele hunichanganyi naye

Funganya funganya funganya funganya

Kibiriti Upele hunifunganyi naye

Shindana shindana shindana shindana

Kibiriti Upele sishindani naye

Basi usijipe taabu wewe basi

Basi sikutaki tena wewe basi

Basi nenda naye huyo wewe basi

Kufa rwako hufi nami kufa rwako

Kufa rwako hufi name kufa rwako

Nenda kamfuate huyo asiye kuliza jina

Kamfate hana choyo  wala ye muhali hana

Kamfate ana moyo muhimu pa jina

Maarufu kifyagio, yeye jamvi la vijana

Swali lake yeye huyo x3 Una hela hauna

Mwoneni huyo x4 Amekuwa hafungani amejishusha taabani

Apitapita njiani amekosa na imani

Amekuwa hajioni, siye tena wa zamani

Hamo tena hesabuni kama jibwa la sokoni

Amekwisha hafahamu amedoda hafahamu

Mzito hakufahamu,  mimi naye sina hamu

Amtakaye amchukue, mchukue mchukue mchukue

<u>Wimbo 2. **Tupendane Wabaya Waulizane – Mzee Yusuf**</u>

Siku zote wa kuombwa ni Mungu

Yetu sote alopanga ni Mungu

Hawa maadui zetu wanafanya kila hila

Na hili penzi letu linalindwa na Mola

Hatuwapi nafasi tunawapa tuendesha

Hawa wapambe nuksi jeuri tutawaonyesha

Kutwa tunaomba Mungu tunaomba Mungu wasije leta majungu,

Tunapendana kizunguzungu, kwa matamu na machungu

Oh! Mpenzi wangu, wabaya wetu macho wameyakodoa

Oh! tuzidi kuomba Mungu, penzi letu lizidi kuendelea

Honey, nataka unibebe unipeleka kuoga

Sweetie unilishe nishibe hata mlo uso mboga

Kisha unipe kila kitu tulichohalalishiwa

Nami nikupe mavitu we mwenyewe unanijua

Kisha tucheze sebende letu mpaka joto analia

Kwa kila mmoja wetu wakituona tazimia

Tupendane kwelikweli wabaya waulizane,

Unijali nikujali vipembeni wanong'one

Amebani makatili penzi letu wasilione

Liwaume penzi hili vipembeni wanong'one

Liwaume penzi hili na dawa wasizione

Unavyocheza sebende- I love you darling
Akikutaka ni bure- I need you sweety
Ah, ayuni wangu wapuuze hao
Raha ya ulimwengu wapuuze roho,
Wabaya wabaya walimwengu wakitaka lao lazima walitimize

Sweety usiku unibembeleze uje mwema usingizi
Honey taratibu unilaze, tukutane kwenye njozi
Tuwaone wenye wivu watapojitia vitanzi
Wale wenye roho mbovu watakonda kama uzi

Ah! Sisi tuko kwenye malavu, tunafanya makamusi,
Tunakula tunda mbivu kwa manakshi na mapozi

Tupendane kwelikweli wabaya waulizane,
Unijali nikujali vipembeni wanong'one
Amebani makatili penzi letu wasilione
Liwaume penzi hili vipembeni wanong'one
Liwaume penzi hili na dawa wasizione
Unavyocheza sebende- I love you darling
Akikutaka ni bure-
Ah! Habiti wangu usipunguze dozi, mimi bado sijapoa
Daktari wangu dawa zako we ndo zitonisaidia

Ah! Sweety asubuhi nikiwa hoi, wayaja na makamusi
Honey, basi nipe chai yenye nyingi tangawizi

Tupendane kwelikweli wabaya waulizane,
Unijali nikujali vipembeni wanong'one
Amebani makatili penzi letu wasilione
Liwaume penzi hili vipembeni wanong'one
Liwaume penzi hili na dawa wasizione
Unavyocheza sebende- I love you darling
Akikutaka ni bure-

Tutoke tukatanue kokote katika nchi
Kokote wewe nambie waisei Cocobichi
Kisha nitayarishie juizi ya parachichi
Wazushi tuwaringie timu yetu kali kwa mechi
Timu yetu kali kwa mechi

Wawili wakipendana adui hana nafasi
Mbona mtaumwa sana, nyiye wabaya wanafsi
Nuru imetuwakia tunamshukuru Mungu
Wale walotupangia na kutuletea majungu
Mungu atawaungua kwa miiba ya sungu
Pendo tumelizingua kwa yasini tatu
Lisije kuhusudiwa na macho ya watu

Yeye namwamini na kumwacha sithubutu

Mbona mnaumwa sana na ni ngumu kupona

Roho zitasonona

Ni vigumu kuachana eti miye nianze tena

Hawa wanaumwa wanaumwa sana

Wanachomwa wanachomwa sana

Wanachomwa sisi kupendana

Kama mnaweza…………pandeni mwende mkazibe

Oh! Kama mnaweza…….pandeni juu mwende mkazibe

Mwende kwa helikopta……. pandeni juu mwende mkazibe

Kama shubiri ni tamu, asali ina ladha gani?

Huyu kanitia wazimu vinenoneno punguzeni

Oh! Kama mnaweza…….. pandeni juu mwende mkazibe

Mwende kwa helikopta……. pandeni juu mwende mkazibe

Wimbo 3. **<u>Utalijua Jiji – Afua Suleiman</u>**

Kazi yako ufisadi jeuringe bena nongwa

Baraka ya ukhaini ukaalika maembe kwakwa

Ushamba umekuzidi maandazi ukanywia chokwa

Vituko vya maksudi si bure we umerogwa

Badala ya soda baridi ama juisi ya chungwa

Mwenzangu huna ujuzi mpenzi umemwudhi

Kaja kwangu nimempokea kaja kwangu nimempokea

Pokea chako kibomu shoga nakutumia

Hata ukinilaumuu, wako nishamchukua

Penzi ulimdhulumu visa ukamfanyia

Chachandu vitamutamu bwana hukumpatia

Bwana kapata wazimu kashindwa kuvumilia

Kwangu akatia timu tiba nikampatia

Nikampa vitu adimu kwako hajajionea

Amri akasalimu magoti kunipigia

Huku akijilaumu kwako kapotea njia

*Kwako kaachia ngazi kwangu kaweka makazi*

*Sasa bwana kabarizi kachoka yako maudhi*

*Utamaliza mizizi talasimu na hirizi ongeza na vipodozi*

*Kwake hupati nafasi mimi ndiye wake pumzi*

Kapenda yangu nidhamu na utulivu nyumbani

Pamoja na ukarimu kwa ndugu na majirani

Ucheshi na tabasamu kanijalia Manani

Nimepewa lugha tamu nyoka hutoka pangoni

Sifa hizi ni muhimu na mengi mengine ndani

Wewe mkaanga sumu kwako hazipatikani

Na mapishi yako bomu, kitimtimu jikoni

Wali wautia ndimu, hayo ni mapishi gani?

Bwana imemwisha hamu kakutimua nyumbani

Unaningoja njiani madhila kunifanyia

Usitake ushindani hunishindi nakwambia

Mimi naletewa ndani wewe watanga na njia

Magomeni buguruni ndara zakukatikia

Wasela vijueni nafuu wajipatia

Uroda kwa foleni kwako wajipendelea

Wewe gumzo mjini watu wanahadithia

Umeyachika ndoani kwa yako mbaya tabia

Unaogea jikoni bafuni unapikia

Tazama utalijua jiji mwenzangu

Chajio utakunywa uji mwenzangu

Na juisi utakunywa maji mwenzangu

Huyu kwako harudi tena mwenzangu

Na jina basi! na jina basi

Utajijue-ee! Utajiju!

Utajiju, wewe utajiju!

Ni wako nishamchukua kwako harudi tena we mwenzangu --- Oh! Utalia mwenzangu jiji utalijua

Katamka wazi wazi kuwa hakutaki tena we mwenzangu --- Oh! Utalia mwenzangu jiji utalijua

Bwana kanipa nafasi nimwonyeshe ujuzi we mwenzangu ---- Oh! Utalia mwenzangu jiji utalijua

Nami sifanyi ajizi mpenzi namuenzi we mwenzangu --- Oh! Utalia mwenzangu jiji utalijua

Nampikia maandazi na chai ya tangawizi we mwenzangu --- Oh! Utalia mwenzangu jiji utalijua

Wali wa nazi kwa ndizi mavitu vuta makazi --- Oh! Utalia mwenzangu jiji utalijua

Kisha natoa dozi impayo usingizi we mwenzangu ---- Oh! Utalia mwenzangu jiji utalijua

Mwenzangu huna ujuzi rudi tena kajifunze we mwenzangu ---- Oh! Utalia mwenzangu jiji utalijua

Bibi acha upuzi kuishi na mume kazi we mwenzangu ---- Oh! Utalia mwenzangu jiji utalijua

Mume ataka malezi, sio mambo ya kipuzi we mwenzangu--- Oh! Utalia mwenzangu jiji utalijua

Kebe na jeuri zako leo zimekuishia we mwenzangu-----Oh! Utalia mwenzangu jiji utalijua

Oh! Utalia mwenzangu jiji utalijua ---- Oh! Utalia mwenzangu jiji utalijua

Wimbo 4 **<u>Nyaubati – Rukia Juma</u>**

Msogee wa mbali msogee wa mbali Nyaubati anasutwa leo

Nikisema Nyaubati hasutiki siku yake imefika leo tumkomeshe

Nyaubati nyaubati una dira ya kutafuta umbea

wala huoni hasara kwa vile umebobea

Ukishapata dhamira uloikusudia

Waona kama ajira mshahara wangojea

Ukome wako ujura sasa unakuungua

Nyaubati huyo ameunguliwa ameshushuliwa na kungondolewa

Hiyo ngondo Nyaubati anasutwa ----- hiyo ngondo

Nasema hiyo ngondo Nyaubati msuteni ------ hiyo ngondo

Lazima asutwe Nyaubati mpekupeku

Nyaubati umbea wauchorea ramani

Nyaubati kumbakumba utamkumbia nani

Kutwa ni kwenye vijumba umchanganishe nani

Umbea kwako ni shamba walima mazao gani

Ujichambue mshamba uache sisi mjini

Nyaubati hujijui hujioni

Katu mimi hunipati ingia tena chuoni

Kuta ni wa mashariki na walimu wako nani?

Wakupangie na ruti uhangaike mjini

Bure yako mikakati hata ukifanya nini

Hufuti yangu riziki hata ukifanya nini

Una cheti cha ukocha wafundisha timu gani

Nyaubati udondocha na kaufanya kama fani

Wenzio wanakucheka hujiulizi kwa nini

Nyeusi rangi ya kucha aliyekuambia nani

Vipuli kwenye kichwa kama si ushamba nini?

Nyaubati huyo leo tutamkomesha

Huyo hana haya huyo Nyaubati kashushuliwa

Huna lako Nyaubati huna lako umeumbuka

Umeshushuliwa Nyaubati huna haya Nyaubati

Ukome umbea Nyaubati huna haya Nyaubati